




**CAG** abaini tena madudu mikopo ya elimu ya juu

UKURASA 3





# Nipashe

Alhamisi Aprili 14, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580915

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Wadau waomba nauli zipandishwe

**WATAKA** mikoani zipande asilimia 34 hadi 54, LATRA yatoa neno ...*Endelea Uk. 2*




## Ndugai atinga bungeni tangu ajiuzulu, aibua shangwe, vifijo

UKURASA 3



Aliyekuwa Spika wa Bunge na Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai, akisalimiana na baadhi ya wabunge wenzake, baada ya kuingia kwenye ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

## Serikali yatoa msimamo uagizaji huria wa mafuta

UKURASA 2




Ofisa Mkuu wa Wateja binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (kushoto), akimpa maelezo Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kuhusu benki hiyo, ilivyojipanga kuhudumia kilimo, baada ya kutangaza makubaliano ya kushusha riba ya mikopo kwa wakulima, wavuvi na wafugaji kwa asilimia 9, jijini Dodoma jana. Kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Ruth Zaipuna.Habari Uk.7 PICHA: MPIGAPICHA WETU


**MICHEZO** MO DEWJI AITIA MZUKA SIMBA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (katikati), akikabidhi tuzo kwa Balozi wa Uingereza nchini, David Concar, kama sehemu ya kutambua mchango wao katika kuunga mkono kampeni ya Nyumba ni Choo ya Wizara ya Afya, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **Habari Uk. 4. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau waomba nauli zipandishwe

**Na Jenifer Gilla**

KILIO cha wadau wa vyombo vya usafiri kinaonyesha ni dhahiri sasa kwamba nauli za mabasi na daladala zitapandishwa, hivi ndivyo unavyoweza kusema!

Hali hiyo inatokana na wadau hao kukutana jana mkoani Dar es Salaam na kuiomba serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kupandisha bei za usafiri huo, kwa kuwa gharama za maisha zimepanda.

Wamependekeza nauli kuongezaka kwa asilimia 34 hadi 54 kwa mikoani, huku kwa mijini kilometa 10 iwe Sh. 745.00, kilometa 15 (Sh. 1,117.40), kilometa 20 (Sh. 1,490), kilometa 25 (Sh. 1862.50) na kilomita 30 (Sh. 2235).

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi nchini (TABOA), Abdalah Kiongozi, alisema nauli za mabasi yaendayo mikoani zinazotumika kwa sasa zina zaidi ya miaka tisa wakati gharama za vyombo vya usafiri, ilikuwa ndogo, hivyo kuna haja ya kuzibadilisha kwa kuwa sasa zimepanda.

"Nauli zimekuwa chini kwa muda mrefu kwa sababu mara ya mwisho nauli zilirekebishwa mwaka 2013, gharama za maisha zimepanda ukilinganisha miaka hiyo na sasa. Labda nikwambie tu kipindi hicho dola moja ilikuwa ni sawa na Sh.1,596 wakati leo hii dola moja ni Sh. 2,345, kwa hiyo utaona hapo kuwa imepanda kwa takribani asilimia 67," alisema.

Alisema hata gharama za kununulia mabasi nazo zimepanda ukilinganisha na kipindi cha nyuma hadi kufikia Sh. miioni 400 kutoka Sh. milioni 200 kwa mabasi yanayotoka China huku kwa Marcopolo zimepanda hadi Sh. milioni 700, hivyo kuziomba mamlaka kupandisha ili kuendana na kasi hiyo. "Wenzetu ambao wamepeleka mapendekezo wameshauri kuwa nauli iongezeke kuanzia asilimia 34 hadi 54 kulingana na kila kilometa, mfano kama nauli ya Dar kwenda Kigoma kwa sasa ni Sh. 60,000 basi ingestahili iongezeke hadi kufikia Sh. 80,000," alifafanua.

**NAULI ZA DALADALA**

Mwenyekiti wa Umoja wa Wamiliki wa Daladala Dar es Salaam (DARCOBOA), Sabri Mabruk, alisema kwa umbali wa kilometa 10 nauli iwe Sh. 745.00, kilometa 15 (Sh. 1,117.40), kilometa 20 (Sh. 1,490), kilometa 25 (Sh. 1,862.50), kilomita 30 (Sh. 2,235), huku wakipendekeza wanafunzi walipie nusu ya gharama hizo.

Katibu wa Daladala mkoa wa Arusha (DDA), Abdalah Kavinje, alisema lengo la ushiriki wao ni kuieleza LATRA kuwa wakati inapopandisha nauli usiulinganishe mkoa huo na Dar es Salaam kwa sababu mfumo wa uendeshaji ni tofauti. "Kwa barabara ya kilometa kumi abiria wanaopanda wengi wanashuka mwisho wa kituo tofauti na Dar es Salaam ambapo wanashuka na kupanda kabla ya kufika mwisho wa kituo, kwa hiyo kutupangia nauli sawa wanakuwa wanatuumiza sisi wa mikoani,"alisema.

**WATETEZI WA ABIRIA**

Mrakibu wa chama cha kutetea haki za abiria taifa (CHAKUA), Hamis Kassim, alisema wakati wadau wa usafiri wanajadili kupandishwa nauli wafikirie pia suala la kuboresha utoaji wa huduma hizo kwa sababu kwa sasa huduma hiyo si nzuri.

"Ajali zimekuwa nyingi, watu wanakata ruti, sehemu ya nauli ya chini wanapandisha, ya nauli ya juu wanapunguza hamueleweki, wote tufuate kanuni na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria," alisema.

Akifungua mkutano huo, Katibu Tawala wa mkoa wa Dar es Salaam, Hassan Lugwa, alisema lengo la serikali ni kufanya uamuzi wa pamoja bila kuuonea upande wowote, hivyo ujumuishaji wa wadau hao ni muhimu.

Aliongeza serikali inatambua mchango wa wadau wa usafiri nchini kwa kuwa ni jambo ambalo linalogusa sekta mbalimbali kwa hiyo ni muhimu kufanyika uamuzi wenye tija kwa pande zote na wenye kutelezeka kinyume na hivyo kutasababisha kuyumba kwa sekta hizo ikiwamo kupanda kwa bidhaa.

Alitaka wadau wapewe nafasi ya kuainisha vigezo vya kupanda nauli hizo ili iwe kielelezo katika kufanya uamuzi wa mwisho.

Meneja Mawasiliano wa LATRA, Salum Pazzy, alisema jukumu walilolifanya jana ni la kisheria, na kuwa linalenga kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora na endelevu kwa upande wa watoa huduma kulingana na tozo wanazotoa, lakini ili huduma hizo ziwe salama ni lazima watoe tozo sahihi.

# Serikali yatoa msimamo uagizaji huria wa mafuta

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema utaratibu wa uagizaji wa pamoja wa mafuta siyo msahafu, hivyo unaweza kubadilishwa wakati wowote kwa manufaa ya nchi.

January alitoa kauli hiyo jana bungeni alipochangia mjadala wa makadrio ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kwa mwaka ujao wa fedha.

Akizungumzia hoja hiyo iliyoibuliwa na Mbunge wa Gairo, Ahmed Shabiby (CCM) na kuungwa mkono na Mbunge wa Geita, Joseph Musukuma (CCM), waziri huyo alisema serikali iko tayari kumpa ushirikiano mtu yeyote atakayefanikisha upatikanaji wa mafuta kwa gharama nafuu.

Shabiby na Musukuma waliitaka serikali kuruhusu uagizaji huria wa mafuta ufanyike sambamba na ununuzi wa pamoja wa nishati hiyo ili kukabiliana na kupanda kwa bei ya mafuta katika kipindi hiki cha vita kati ya Russia na Ukraine.

January alisema uamuzi huo wa uagizaji wa pamoja wa mafuta ni maelekezo ya Bunge ya mwaka 2011, kwamba kipindi hicho wabunge kwa kauli moja walishauri uagizaji ufanyike kwa utaratibu huo na umekuwapo kwa takriban miaka 10 , umewekwa na watu na unatumiwa na watu. "Tumepokea ushauri wa wabunge na tutaufanyia kazi ili kuuboresha mfumo huu. Mfumo huu si msahafu, unaweza kubadilishwa wakati wowote pale tunapoona kuna manufaa kwa nchi. Kikubwa ni kupata unafuu wa kupata mafuta.

"Wapo wabunge wamesema wana uwezo wa kupata mafuta huko baharini kwa bei nzuri. Mtu yeyote anayeweza kuleta mafuta kwa bei nafuu, karibu sana ofisini hata leo. Hatuwezi kung'ang'ania kitu kimoja wakati kuna kitu kingine kinaweza kutusaidia zaidi.

"Ndugu zangu, kuweka mafuta kwenye vigaloni majumbani ni hatari, mafuta ya kutosha yapo juu ya kiwango tulichoweka cha utoshelevu wa siku 15," alisema.

**MISHAHARA SEKTA BINAFSI**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, akizungumzia hoja ya Mbunge wa Vwawa, Japhet Hasunga (CCM), kuhusu kurekebisha kima cha chini ya mishahara ya Sekta Binafsi, alisema ameunda bodi ya mishahara kwa sekta hiyo.

Aliwaomba waajiri wote nchini watoe ushirikiano kwa bodi hiyo ili ifanye utafiti na kutoa ushauri kwa serikali ili kupanga kima cha chini ya mishahara kwa sekta binafsi.

Prof. Ndalichako pia aliahidi kufuatilia kwa kina na kulipatia ufumbuzi tatizo la kuchelewa kwa malipo ya mafao ya wastaafu, akisisitiza "watu wameitumikia nchi kwa moyo, wanapomaliza utumishi wao, lazima wapate stahiki zao bila usumbufu wowote."

**ELIMU KWA MPIGAKURA**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), George Simbachawene, alisema moja ya mikakati ya kuongeza idadi ya wapigakura ni kuhakikisha elimu inatolewa ili wahamasike.

Aliziomba taasisi, asasi za kiraia na viongozi wa kijamii kushiriki kuhamasisha elimu kwa wapigakura ili kuwa na wapigakura wengi zaidi katika uchaguzi ujao na kwamba daftari la wapigakura litafanyiwa marebisho mara mbili kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu mwingine kwa mujibu wa katiba. Simbachawene pia aliitaka jamii kuunga mkono jitihada za serikali za kupiga vita matumizi ya dawa za kulevya, akibainisha kuwa kwa sasa matumizi ya bangi yamekuwa kama fasheni kwa wanawake.




Mtaalam wa Kilimo cha Parachichi, wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa, Paschal Chengula, akitoa mafunzo ya kilimo bora cha parachichi kwa vijana 100, wanufaika wa mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM) katika kata ya Luhunga, wilayani humo, jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# CAG abaini madudu mikopo elimu ya juu

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini dosari katika mchakato wa utoaji wa fedha za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ikiwa ni pamoja na kutopewa nafasi kwa vijana wanaotoka familia zenye kipato duni.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa juzi, CAG Charles Kichere anasema alipitia orodha iliyotolewa ya wanafunzi walio chini ya uhitaji ili kuthibitisha kama mikopo inatolewa kulingana na mahitaji na kubaini kuwapo kwa dosari katika mgao wa waombaji 12,660.

CAG anafafanua kuwa alibaini waombaji waliopata mikopo chini ya uhitaji wao, waliopata mikopo lakini wakiwa na uhitaji hasi na waliopata mikopo mikubwa kuliko mahitaji yao.

"Pia, wakati nikichambua orodha ya wanafunzi waliopimwa uhitaji wa mkopo kwa mwaka wa masomo 2020/21, nilibaini wanafunzi 71 kutoka kaya maskini zenye kipato cha chini na walio katika Mpango Maalum wa Kusaidia Uchumi (TASAF) walidahiliwa katika vyuo vikuu mbalimbali lakini hawakupangiwa mikopo.

"Kutokukithi mahitaji kwa mchakato wa ugawaji wa mikopo kunachangiwa na ukweli kwamba uthibitishaji wa maombi hufanywa kabla ya mchakato wa ugawaji wa mikopo.

"Pia, kutowasilisha wanafunzi waliodahiliwa kwa wakati kunaweza kusababisha ugawaji mbaya wa mikopo kwa waombaji wenye uhitaji.

"Nina wasiwasi kuwa ucheleweshwaji wa udahili wa wanafunzi unaweza kusababisha kukosa mkopo kwa waombaji wanaostahili au kinyume chake. Pia, kunaweza kusababisha waombaji wanaostahili kukosa mikopo hiyo kwa sababu ya ufinyu wa bajeti," anasema.

Katika mapendekezo yake, CAG anasema uongozi wa HESLB ufanye ukaguzi wa udhibiti wa mfumo wakati wa mchakato wa ugawaji wa mikopo na kuchukua hatua stahiki ili kufanya mchakato huo kuwa na ufanisi zaidi.

**TAARIFA ZA WAAJIRI**

CAG pia anasema amebaini kutokuwapo taarifa za kutosha za mwajiri na wakopeshwaji kwa ajili ya ufuatiliaji wa mkopo, akifafanua kuwa wakati wa ukaguzi, alihoji kuhusu kuwapo kwa orodha ya waajiri na alipitia ili kuthibitisha usahihi na ukamilifu wa taarifa za waajiri kwa ajili ya ufuatiliaji mzuri wa wanufaika wa mikopo.

Anasema kuwa HESLB ilitoa orodha ya waajiri 6,840 lakini mapitio yalibaini kuwa orodha ya waajiri ina rekodi zisizo kamili na kwamba katika orodha hiyo, hakukuwa na namba ya mlipakodi kwa waajiri wote, waajiri 150 hawakuwa na anwani wala namba za simu.

"Zaidi, hakukuwa na kipengele cha taasisi kama ilivyobainishwa katika mwongozo kama vile balozi za Tanzania, balozi za nje, kamisheni kuu, kampuni, wamiliki wa biashara.

"Pia, nilipitia kanzidata ya wakopeshwaji katika mfumo wa LMS ili kubaini ukamilifu wa maelezo dhidi ya mahitaji ya mwongozo ambapo nilibaini kuwa baadhi ya taarifa zinazohitajika hazikuwa kamilifu. Taarifa hizo ni kama vile namba ya simu, barua pepe na anwani za mahali," anasema.

# ...aanika uhaba watumishi Muhimbili

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini kuwapo dosari ya uhaba wa watumishi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), unaoathiri utoaji wa huduma hospitalini huko.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa juzi, CAG Charles Kichere, anasema ikama ya MNH kwa mwaka wa fedha 2020/21 inaonyesha uhitaji wa wafanyakazi 4,567.

Hata hivyo, hadi kufikia wakati wa ukaguzi huo mwezi Novemba 2021, hospitali hiyo ya ngazi ya juu zaidi nchini ilikuwa na jumla ya watumishi 2,734 ikiwa na upungufu wa watumishi 1,833 (asilimia 40).

CAG anafafanua kuwa kitengo cha uzazi kina upungufu wa watumishi 171, wodi ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU) ina upungufu wa watumishi 124, wodi ya watoto (124), idara kuu ya upasuaji (83). "Nilibaini pia kuwa nafasi za ajira mpya 485 ziliidhinishwa kati ya mwaka wa fedha 2017/18 na 2020/21 na Ofisi ya Rais Utumishi ambapo kati ya nafasi hizo, vibali vilivyotolewa kuajiri watumishi wapya ni 248 pekee kati ya nafasi zilizoidhinishwa.

"Upungufu huu ulisababishwa pia na kuondolewa kazini kwa wafanyakazi waliokuwa na vyeti feki. Upungufu huu wa wafanyakazi unaweza kuathiri ubora wa utoaji wa huduma hospitalini," anasema.

Katika mapendekezo yake kuhusu suala hilo, CAG anasema menejimenti ya Hospitali ya Taifa Muhimbili ifuatilie Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa nia ya kuhakikisha nafasi zilizo wazi zinajazwa.

# Ndugai atinga bungeni, aibua shangwe na vifijo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BAADA ya kutoonekana kwa muda mrefu bungeni, aliyekuwa Spika wa Bunge na Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai, jana aliingia bungeni kwa mara ya kwanza tangu alipotangaza kujiuzulu wadhifa huo Januari 6, mwaka huu.

Hatua ya kiongozi huyo kuhudhuria mkutano wa Bunge la bajeti unaoendelea jijini hapa, iliibua shangwe na vifijo kutoka kwa wabunge wenzake, baada ya Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kutangaza uwapo wake.

Kuingia kwa Ndugai jana kulihitimisha siku 98 tangu alipochukua uamuzi huo na ikiwa ni mara ya pili kuonekana hadharani toka wakati huo, mara ya kwanza ikiwa ni juzi katika tukio la uzinduzi wa chanjo wilayani Kongwa.

Tangu ilipotangazwa amejiuzulu nafasi ya Spika, Ndugai alikuwa hajaonekana bungeni, akikosa mkutano wote wa sita wa Bunge la 12 uliofanyika kwa wiki tatu Februari, mwaka huu, huku kukiibuka maswali kuhusu alikokuwa.

Hata hivyo, uongozi wa Bunge kupitia Ofisi ya Katibu wa Bunge ulipoulizwa na Nipashe, ulibainisha kuwa Ndugai alikuwa jimboni Kongwa katika kipindi hicho ambacho alikuwa haonekani bungeni wakati wabunge wenzake wakiwa wanaendelea na mkutano wa Bunge la Bajeti.

Jana saa 2:30 asubuhi Ndugai aliingia bungeni ambapo wabunge mbalimbali walionekana wakimfuata kumsalimia kwenye kiti chake.

Baada ya kipindi cha maswali na majibu kuisha, akitambulisha wageni, Spika Tulia alisema "Kwa namna ya kipekee kabisa, nitambue uwapo wa Job Yustino Ndugai."

Spika Tulia alipomtambulisha, Ndugai alisimama na kuwapungia mikono wabunge huku wakimpigia makofi ya kibunge kwa kupiga meza huku baadhi yao wakipiga vigelegele.

Akiendelea kumtambulisha, Spika alisema: "Haya asanteni sana waheshimiwa wabunge kwa heshima hiyo mliyompa Spika Mstaafu ambaye yupo nasi siku ya leo. Karibu sana Mheshimiwa Mbunge mwenzetu."

Mara ya mwisho Ndugai kuvaa joho la Spika na kuongoza kikao cha Bunge ilikuwa Novemba 12, mwaka jana, siku ambayo pia ulikuwa ukomo wa Mkutano wa Tano wa Bunge la 12.

Hii ina maana kwamba Ndugai hakuhudhuria vikao vyote vya Mkutano wa Sita wa Bunge la 12 vilivyofanyika Februari, mwaka huu, na jana ameanza kuhudhuria vikao vya Mkutano wa Bunge la Bajeti ambavyo vilianza Aprili 5.


**ABBOTT FUND TANZANIA**
**(Company No. 58641)**
**(Certificate of Compliance No. 1828)**

**PUBLIC NOTICE MADE PURSUANT TO REGULATION 13 (A) OF THE NON-GOVERNMENTAL ORGANISATION ACT (AMENDMENTS) REGULATIONS 2018 MADE UNDER GOVERNMENT NOTICE NO. 609 OF 19TH OCTOBER 2018**

**WHEREAS** Regulation 13 (a) of the abovementioned regulations require that all non-governmental organisations in Tanzania publish biannually funds received and their expenditure in a widely circulated newspaper which are accessible by the targeted beneficiaries as part of financial transparency and accountability compliance requirements.

**IN VIEW OF THE ABOVE,** we wish to make the following public disclosure of the funds received in 2021 and their expenditure, which publication covers the reporting period from 1st January 2022 to 30th June 2022:

| Project Area Expenditure | Amount in (USD) |
|---|---|
| **Muhimbili National Hospital Sustainability Strategy Support:** Includes support to Leadership Capacity-Building | 384,000 |
| **Emergency Medicine Regional and District Amplification:** Includes support to MNH Emergency Medicine; Infrastructure project at Chalinze District Hospital | 793,000 |
| **Village Emergency Care Model** | 136,000 |
| **Building Livelihoods:** Includes National Children's Centre Infrastructure Project (Dodoma) | 350,000 |
| **Administration:** Includes travel, office costs and program implementation staff | 1,744,000 |
| **Total Funds received from Abbott Fund, Chicago IL, USA for the year 2021** | **3,407,000** |

**ISSUED BY**
**EXECUTIVE DIRECTOR**
**ABBOTT FUND TANZANIA**

# Waziri Mkuu ataja hatua kukabili ugumu wa maisha

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametaja hatua zinazochukuliwa na serikali kukabiliana na kupanda kwa bei za bidhaa nchini.

Akihitimisha hoja ya makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa mwaka 2022/23, Waziri Mkuu alisema serikali itaendelea kuhakikisha bei ya bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi zinakuwa himilivu.

Majaliwa aliitaja hatua ya pili kuwa ni serikali kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa nje ya nchi, kupitia kamati zake za bei za mikoa na wilaya, zitaendelea kufanyiwa tathmini kuona namna ya kuleta unafuu katika masoko.

"Kamati hizi zinazoongozwa na wakuu wa wilaya na mikoa, ndiyo wenye wajibu wa kupita katika masoko yetu kuona bidhaa zilizopo, zile zinazozalishwa ndani ambazo hazina sababu ya kupandishwa bei zitakuwa zinadhibitiwa na kamati ya bei ya ngazi ya wilaya na mkoa," alisema.

Waziri Mkuu pia alisema serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi hususani wazalishaji na wasambazaji wa bidhaa ili kupanga viwango vipya vya bei vitakavyoleta unafuu kwa mlaji na kuhakikisha zinapatikana.

"Lakini pia kupunguza gharama za vifaa vya usafiri na usafirishaji ambazo zimekuwa na athari ya moja kwa moja kwenye kupanda kwa bei ya bidhaa," Majaliwa alisema.

Waziri Mkuu alisema kupungua kwa bei za bidhaa kunategemea kushushwa kwa bei ya bidhaa zingine ndani ya masoko.

Majaliwa alisema serikali itaendelea kuimarisha uzalishaji wa bidhaa za viwandani hasa za chakula zinazoingizwa kwa wingi kutoka nje ya nchi ikiwamo ngano, mafuta ya kula na sukari kwa kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji kwa kutoa vivutio stahiki vya uwekezaji.

Alisema serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwenye uwekezaji wa ndani wa bidhaa na huduma mbalimbali ili kukabiliana na aina hiyo ya mtikisiko wa kiuchumi.

"Lakini pia serikali itaendelea kufanya mapitio ya kisera za kibiashara ili kuona maeneo yanayoweza kuleta nafuu katika nchi," alisema.

Majaliwa aliiagiza Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuangalia bei katika masoko na kuchukua hatua kwa wakati sambamba na kusimamia vyema mfumo kupokea taarifa kutoka kwa wananchi kuhusiana na mwenendo usioridhisha wa bei za bidhaa sokoni.

Pia aliagiza kamati za bei na biashara za wilaya na mikoa zihakikishe zinafuatilia katika masoko na kuhakikisha kuwa zinajiridhisha kuhusu kupanda kwa bei katika kwenye maeneo yao.

Majaliwa aliagiza mamlaka za serikali za mitaa na taasisi zilizopewa dhamana ya kusimamia mwenendo ya bei katika masoko ya bidhaa kutekeleza wajibu wao kikamilifu na kwa makini sambamba na kudhibiti vitendo vya upandishaji wa bei holela.

"Nitumie nafasi hii kukemea vitendo vya wafanyabiashara na wazalishaji wasio waaminifu kupanga bei, kufanya migomo, kukubaliana katika ununuzi na kuuza kwa bei ya juu, mbinu ambazo wakati mwingine zimekuwa ni chanzo cha kupanda kwa bei ya bidhaa," alionya.

# CAG abaini ubambikizaji bili za maji kwa wananchi

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini dosari kuwapo tatizo la wateja wa mamlaka za maji kubambikiwa bili kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za kimfumo.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa juzi, CAG Charles Kichere anasema amebaini Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ilitoza bili za maji kwa wateja 1,207 na kupata mapato ya Sh. milioni 755.65 bila kusoma mita za maji kwa matumizi ya maji ya kila mwezi.

Anafafanua kuwa kati yao, wateja 371 walikuwa na mita mbovu, hivyo walitozwa gharama za maji kwa makadirio; na wateja 836 walitozwa gharama za huduma za majitaka kwa kukadiria kwa kuwa hawakuwa na huduma ya maji safi.

Katika hilo, CAG anafafanua kuwa matumizi ya maji safi yangeweza kutumika kukadiria gharama za majitaka na kwamba yote hayo ni kinyume cha Aya ya 1.8.2 ya Mwongozo wa Huduma kwa Wateja wa Mamlaka unaotaka matumizi ya maji kubainishwa kwa kutumia usomaji halisi wa mita; na kinyume cha Aya ya 1.8.3 ya mwongozo huo unaoelekeza kuwa endapo kuna mita ambazo hazijasomwa, usomaji unapaswa kukadiriwa kulingana na usomaji wa zamani na makisio hayo yabadilishwe mara baada ya kufanya usomaji halisi kwa mita husika.

"Nina shaka na kutokusanywa kwa kiasi kilichotozwa na kiasi kinachotozwa kwa makadirio kwa sababu wateja wanaweza kulipa zaidi au pungufu ya kiasi kinachotakiwa, hivyo kusababisha upotevu wa mapato.

"Ninapendekeza DAWASA kuhakiki na kufunga mita kwa wateja wote wanaopatiwa maji na kuhakikisha mita zinasomwa na mapato yanakusanywa ipasavyo," CAG anatahadharisha.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

## AUDITED RESULTS

FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2021

**CHAIRMAN'S STATEMENT**

Tanzania Portland Cement Public Limited Company (TPCPLC) continues to deliver strong results compared to prior years. Revenue increased by 14.2% compared to year 2020. This increased revenue, combined with cost optimization led to an increase in operating profit of TZS 125.6bn versus TZS 104.9bn in 2020.

| INCOME STATEMENT | 2021 TZS'000 | 2020 TZS'000 |
|---|---|---|
| Revenue | 449,509,301 | 393,739,558 |
| Cost of sales | (293,185,036) | (261,389,401) |
| **Gross profit** | **156,324,265** | **132,350,157** |
| Other operating income | 1,205,920 | 2,250,391 |
| Selling and administrative expenses | (3,010,835) | (2,942,285) |
| Administrative expenses | (23,514,168) | (23,003,381) |
| Other operating expenses | (5,423,601) | (3,709,781) |
| **Operating profit** | **125,581,581** | **104,945,101** |
| Financial items | 2,455,607 | 2,484,133 |
| **Profit before tax** | **128,037,188** | **107,429,234** |
| Taxes on income | (39,555,603) | (32,752,864) |
| **Profit for the year** | **88,481,585** | **74,676,370** |
| Other comprehensive income , net of tax | (1,076,842) | 1,028,800 |
| **Total Comprehensive Income** | **87,404,743** | **75,705,170** |
| Number of Shares | 179,923,100 | 179,923,100 |

| BALANCE SHEET | 2021 TZS'000 | 2020 TZS'000 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| Intangible fixed assets | 1,006,537 | 797,216 |
| Tangible fixed assets | 145,850,876 | 134,429,769 |
| Right of use assets | 982,483 | 4,198,644 |
| Non-current financial assets | 796,000 | 1,346,000 |
| **Non.current assets** | **148,635,896** | **140,771,629** |
| Inventories | 52,935,487 | 52,404,781 |
| Trade and other receivables | 62,864,186 | 55,571,973 |
| Other current financial assets | 600,000 | 600,000 |
| Cash and cash equivalents | 114,278,364 | 103,855,770 |
| **Current assets** | **230,678,037** | **212,432,524** |
| **TOTAL ASSETS** | **379,313,933** | **353,204,153** |
| **EQUITY & LIABILITIES** | | |
| **Equity** | **272,235,501** | **255,000,767** |
| Lease liabilities | 186,758 | 1,231,231 |
| Long term provisions | 7,739,484 | 6,337,102 |
| Provision for deferred taxes | 11,618,859 | 14,273,690 |
| **Non-current liabilities** | **19,545,101** | **21,842,023** |
| Lease liabilities | 1,044,405 | 3,725,915 |
| Current income tax payable | 28,859 | 1,013,768 |
| Trade and other payables | 83,611,599 | 68,765,217 |
| Dividend payable | 2,848,468 | 2,856,463 |
| **Current liabilities** | **87,533,331** | **76,361,363** |
| **TOTAL EQUITY & LIABILITIES** | **379,313,933** | **353,204,153** |

The operating performance of the plant and availability of the equipment was good, and sales volume, clinker and cement production during 2021 achieved record levels. The continued focus on customer centricity and production of high-quality products enabled TPCPLC to remain the leading player in the industry.

**Prospects**

The cement demand in Tanzania and the East-African region has been growing steadily in recent years and still today. TPCPLC is well placed to meet this growing demand and continue to produce high-quality products.

TPCPLC continues to make progress toward its sustainability policies, particularly environmental and carbon emissions targets. This includes increasing biomass usage in clinker production.

**Dividend**

The Board proposes a cash dividend for the year 2021 of TZS 390 per share. The Register of Members will close on 13 May 2022, and the last day of trading cum dividend will be 9 May 2022. The dividend will be paid on or about 30 June 2022.

**Appreciation**

The Board would like to thank all its stakeholders for their support during the past year. We have every confidence that TPCPLC will continue to deliver value for the shareholders in the future.

BY ORDER OF THE BOARD

Hakan Gurdal
Chairman of the Board
13.04.2022

**Tanzania Portland Cement Public Limited Company**
**P.O.Box 1950**
**Dar-es-salaam**
**Tanzania**
**www.twigacement.com**
**Email: info@twigacement.com**




# Bado siamini nimeshinda karibu TSh89 Milioni betPawa

**Mimi ni Fariji kutoka Nachingwea na nilibeti TSh250 kwenye michezo 19 na nikashinda TSh46,821,527. Hiyo iliongezwa hadi TSh88,961,151.30 (kabla ya kodi) kwa Bonasi ya Ushindi ya 90% ya betPawa.**
**Hii ni hadithi yangu...**

Bonasi ya ushindi ya betPawa ndiyo bora zaidi na hakuna anayekaribia hilo.

Nilipata nafasi moja tu kuangalia mkeka wangu na nikaona kila kitu kinaendelea vizuri na sikutakaku Cashout.

Baadaye, nilikua nikiweka pesa katika account yangu ghafla nikaona tarakimu nyingi katika account. Kweli nimeshinda. Sikuamini na bado siamini.

Nataka kununua ardhi na kuanzisha mashamba ya korosho. Ushindi wangu unaonyesha inawezekana, siku moja inaweza kukutokea. Nimeshinda kitu ambacho sikuwahi kufikiria maishani mwangu.

**Pata nafasi ya kujishindia KIKUBWA leo kwenye betpawa.co.tz**

betPawa

CHEZA KIASI. 18+. BETPAWA IMESAJILIWA CHINI YA BODI YA MICHEZO YA KUBASHIRI YA TANZANIA. LESENI #SBI000000026.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali ipunguze matumizi kuwasaidia wananchi wake

**BEI** ya mafuta ya magari imepanda kwa kiasi kikubwa katika historia ya Tanzania, hali iliyosababisha bidhaa nyingine kupanda na kuwapo mfumuko wa bei, na kuathiri maisha ya wananchi wa kawaida.

Wengi wamepaza sauti kuitaka serikali ibane matumizi ili iweze kuingiza ruzuku kwenye mafuta yashuke bei na kudhibiti mfumuko, lakini serikali imekuja na mkakati wa kupunguza kodi ya ndani kwenye baadhi ya bidhaa, huku ikionya wafanyabiashara wanaotumia mwanya huo kupaisha bei. Tunatambua kazi nzuri iliyofanywa ya kuja na mkakati wa kupunguza kodi na kufuatilia wafanyabiashara wanaotumia mwanya huo kupandisha bei, lakini tunaona hizo bado hazitoshi, ni muhimu kwa serikali kuangalia matumizi yake ya kila siku, ili kuwasaidia wananchi kupunguza makali ya maisha.

Pamoja na jitihada hizo, kuna mambo ya msingi ambayo ni lazima serikali iyaangalie ikiwamo kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ambayo kwa sasa yanaonekana yakianza kurejea, jambo linalozua minong'ono kwa walipa kodi. Mathalani, hafla za kitaifa zinaongezeka na viongozi kukusanyika eneo fulani kwa ajili ya jambo fulani, utengenezaji wa fulana, kofia na kanga kwenye shughuli hizo umerejea na watu kutumia mwanya huo 'kupiga' fedha.

Kunapokuwa na halfa ya kitaifa inayohudhuriwa na viongozi wa kitaifa maana yake watakuwapo wa mikoa, wilaya, taasisi mbalimbali na walinzi wao ambao watatakiwa kulipwa posho za kujikimu, magari na watoa huduma kama za chakula, vifaa vya umeme na mabango mbalimbali, vyote hivyo vinahitaji fedha ambazo huenda hazikuwa kwenye bajeti.

Viongozi wengi ni wenye hadhi ya kusafiri kwa ndege na wengine magari yao ambayo hutumia mafuta mengi, maana yake kwa mwezi kukiwa na hafla kama hizo kumi yote ni matumizi makubwa ambayo yanatokana na kodi za wananchi.

Semina, makongamano na mikutano yenye kukusanya viongozi wengi inaifanya serikali kuongeza gharama ambazo zinabebwa na wananchi kupitia kodi zao.

Kama haitoshi kuna gharama za mavazi na muda wa maongezi kwa viongozi wa hadhi fulani, huku wengine wakilipiwa hadi wasaidizi wa nyumbani na sehemu nyingine, yote haya ni matumizi ambayo yangeweza kuzuiwa ili yasaidie wananchi kupunguza makali ya maisha.

Ni kawaida kwa fedha nyingi kuelekezwa kwenye mishahara na matumizi mengineyo, ikiwamo posho na chai za watendaji kuliko kwenye miradi ya maendeleo, jambo ambalo linatufanya tuzidi kurudi nyuma badala ya kuwekeza kwenye huduma muhimu za kijamii.

Katika dunia ya sasa yenye maendeleo ya teknolojia, kalenda za kutundika ukutani hazina umuhimu kwa sababu kwenye simu janja hata vitochi, zinapatikana.

Ni lazima serikali ifanye tathmini kwa kupunguza matumizi makubwa ambayo yanaonekana bila kutajiwa kiasi cha fedha kilichotumika kama hafla nyingi, makongamano, semina na mikutano, kutengeneza vipeperushi.

Kama ingekuwa inawekwa wazi matumizi ya safari za kwenda kwenye kusanyiko fulani kwa viongozi wa kitaifa hadi wilayani, kwa mwezi ni matumizi makubwa ambayo tunaamini yangeelekezwa kusaidia wananchi kupunguza makali ya maisha tungeona mabadiliko.

Pamoja na mikakati iliyotangazwa na serikali ya kupunguza kodi, lakini ni muhimu tuone hata viongozi na serikali kwa ujumla inapunguza matumizi, inapoonekana hali ni ile ile wananchi wanaona wako wenyewe katika kukabili hali ngumu waliyonayo.

Tunaamini kwenye kubana matumizi kutaokoa fedha nyingine kupotea, na zitakwenda kuwasaidia wananchi kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo kuiwezesha serikali kuondoa Sh. 100 kwenye kila lita moja ya mafuta ili angalau bei ishuke.

Kwa sasa wasafirishaji wanataka nauli zipande kwa kuwa gharama za uendeshaji zimepanda, jambo ambalo halikwepeki na ikiwi hivyo maana yake gharama za maisha zitazidi kuongezeka na haijulikana vita itaisha lini, na hata ikiisha kutakuwa na kazi ya kushughulikia matokeo ya vita husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hili la kila kaya iwe na choo bora lingefaa liwe la lazima

**MIKOA** ya Kilimanjaro, Iringa na Njombe, imetajwa kuwa vinara wa kampeni ya miaka mitano ya uhamasishaji vyoo bora na kuvitumia, yenye jina la 'Usichukulie Poa Nyumba ni Choo' iliyohitimishwa Jumatatu wiki hii.

Kilimanjaro imetajwa kuongoza kwa usafi wa vyoo kwa asilimia 89, ikifuatiwa na Iringa asilimia 87.7 na Njombe asilimia 86, halmashauri zikiwa ni Njombe asilimia 100, Iringa asilimia 86.6 na Moshi asilimia 85.

Kampeni hiyo ilianza mwaka 2017 wakati huo kukiwapo asilimia 37 tu ya kaya zenye vyoo bora, lakini sasa zimeongezeka kufikia asilimia 72.1, huku ikielezwa kuwa bado baadhi ya Watanzania hawathamini choo.

Wakati kukiwapo ongezeko la kaya zinazotumia vyoo bora, hali hiyo pia inaelezwa kuwa imesaidia kupungua idadi ya wanaojisaidia vichakani, kutoka asilimia 5.7 na kushuka hadi kufikia asilimia 1.4.

Hayo ni kwa mujibu wa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu wakati akihitimisha kampeni hiyo ya miaka mitano Dar es Salaam, huku ikielezea utafiti wa Benki ya Dunia unavyoonyesha.

Kwamba, Tanzania hupoteza Dola za Kimarekani milioni 200 kila mwaka kwa sababu ya magonjwa yatokanayo na uchafu, hivyo anahimiza umuhimu wa kuwa na vyoo bora na kuvitumia.

Waziri anasema choo ni sehemu ya kwenda kutolea msongo wa mawazo na panatakiwa pawe safi, ambapo anawataka Watanzania kuzingatia ujenzi wa vyoo bora na kuvitumia, huku wakihakikisha vinakuwa safi wakati wote.

Anafafanua kwamba, kuna awamu nyingine ya uhamasishaji wa ujenzi wa vyoo bora itakayofuata baadaye, hivyo kwa maelezo hayo, akidhani ingekuwa vyema kila kaya kuwa na choo bora ingekuwa ni lazima.

Pia, upo umuhimu zaidi wa wataalamu, ikiwa ni pamoja na maofisa afya kuhakikisha elimu na uhamasishaji wa kila kaya kuwa na choo bora inaendelea kutolewa zaidi, na upatikanaji wa vifaa vya kutosha na vya bei nafuu vinavyohitajika katika ujenzi na matengenezo ya vyoo bora na nafuu.

Uhamasishaji wa kitaifa wa mabadiliko ya kimwenendo katika matumizi sahihi ya vyoo na usafi wa mazingira ambao unaratibiwa na Wizara ya Afya, unalenga kudhibiti tatizo hilo la ukosefu wa vyoo bora.

Hivyo, ili kukabiliana na changamoto hiyo, jitihada za makusudi zinahitajika katika kuongeza umuhimu na uhitaji wa vyoo bora miongoni mwa wananchi kwa kusisitiza zaidi ujenzi na matumizi sahihi ya vyoo bora.

Mikoa inayojigundua bado imebaki nyuma katika hilo, haina budi kujifunza kwa mingine iliyofanya vizuri, kwani vyoo bora vina mchango mkubwa katika kulinda afya za watu na jamii kwa ujumla.

Kiafya, inaelezwa kuwa vinasaidia kujenga uchumi imara.

Hiyo inatokana na kwamba, ukosefu wa huduma hizo katika maeneo ya kazi na majumbani, una madhara ikiwamo upunguzaji wa uzalishaji, hivyo umuhimu wake ni mkubwa kuanzia nyumbani hadi sehemu za kazi.

Tumesikia taarifa iliyotolewa na Waziri kuhusu kampeni hiyo ya miaka mitano akielezea mafanikio na changamoto zake ikiwamo baadhi ya mikoa kufanya vizuri kwenye suala la usafi wa vyoo.

Mafanikio hayo ndiyo yanayonishawishi nishauri mikoa mingine kujifunza kitu kutoka kwa ile iliyofanya vizuri, ili ikiwezekana, ichukue mbinu na kuzitumia, ili hatimaye kila kaya iwe na choo bora.

Si kuwa na choo bora tu bali na kukitumia, kwani wakati wa kampeni kulikuwapo na taarifa kuwa baadhi ya kaya zinajenga vyoo bora, lakini hazivitumii, kwa sababu ya mambo ya mila na desturi.

Nina amini kwamba Watanzania wengi wanajua umuhimu wa kuwa na vyoo bora, lakini inasikitisha kuona baadhi katika suala hilo, hawajatoa kipaumbele katika jamii zao kwa sehemu kubwa.

Upo msemo 'Nyumba haikamiliki pasipokuwapo na choo' lakini msemo huu ni kama umebaki zaidi maneno kuliko matendo, hivyo kampeni ya 'Usichukulie Poa Nyumba ni Choo' ingesaidia kuwaamsha.



Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania Plc, Sitholizwe Mdlalose (kulia), akipata maelezo kuhusu bidhaa za simu na vifaa vyake, alipotembelea kwenye moja kati ya maduka ya bidhaa hizo, ikiwa ni sehemu ya ziara ya kukagua masoko ya kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mkuu wa Mauzo wa Vodacom Kanda ya Pwani na Dar es Salaam, Brigita Shirima. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabilioni yamwagwa kukiboresha kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKAKATI wa kusukuma mbele sekta ya kilimo umepata nguvu, baada ya serikali kuingia mkataba utakaowezesha kupatikana kwa Sh. bilioni 120.

Wizara ya Kilimo na Benki ya NMB, wameingia makubaliano ya kukuza sekta hiyo, ambapo benki hiyo imetenga Sh. bilioni 20 kwa ajili ya kutoa mikopo ya ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mazao hasa maeneo ya vijijini na shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kukuza kilimo nchini. Akizungumza katika hafla ya makubaliano hayo iliyofanyika jana jijini Dodoma, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna alisema kuwa wamekubali kuingia makubaliano hayo baada ya mazungumzo ya muda mrefu kati ya Benki hiyo na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe.

Alisema mikopo hiyo ya ujenzi wa maghala ,itatolewa kwa riba nafuu ya asilimia 9 na mazao yanayolengwa kwa kuanzia ni korosho, pamba na nafaka.

Alisema mkopo huo ni mwendelezo wa juhudi ya NMB kuinua sekta ya kilimo nchini kwani Oktoba mwaka jana, benki hiyo ilitenga shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kukopesha sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi kwa riba isiyozidi asilimia 10. "Kwa taarifa tu, mpaka sasa zaidi ya shilingi bilioni 80 zimeshatolewa kwenye mikopo hii. Baada ya kuona shilingi bilioni 100 zinaisha, leo

tunaona tuongeze nyingine kama hizo ili kuongeza utoaji wa mikopo kwa wakulima, wavuvi, wafugaji na wajasiriamali katika sekta hizi huku tukipunguza riba ya mikopo hii mpaka asilimia 9," alisisitiza Zaipuna.

Alisema nyongeza hiyo ya shilingi bilioni 100 kwenye mikopo na shilingi bilioni 20 kwenye ujenzi wa maghala, kunafanya kiasi ambacho tayari kimetengwa na NMB kwa ajili ya mikopo nafuu ya kilimo kufikia shilingi bilioni 220.

"Leo tupo hapa na Waziri wa Kilimo mheshimiwa Hussein Bashe ili kuwatangazia makubaliano tuliyofikia kati ya wizara ya kilimo na benki ya NMB yanayolenga kuendeleza juhudi za kukuza kilimo nchini."

Waziri Bashe aliipongeza NMB kwa juhudi zake za kukuza sekta ya kilimo nchini. Alisema moja ya changamoto wanayokabiliana nayo wakulima vijijini ni mazao yao kupoteza ubora kabla ya kufika sokoni kutokana na mazingira mabaya ya kuhifadhi mazao yao.

"Kule vijijini ukiona magunia mengi ya mazao yamewekwa kwenye eneo la mashine za kusaga, usifikiri kuwa ni mali ya mwenye mashine hiyo.

Magunia hayo ni mali ya wakulima yamehifadhiwa hapo baada ya kukosa ghala la kuhifadhia na yanapofika sokoni, yanakuwa yamepoteza ubora na thamani yake," alisema Bashe.

Alisema wizara yake inatambua matatizo na changamoto za wakulima na imejipanga kukabiliana nayo kwa kushirikiana na wadau kama Benki ya NMB.

# RC Kafulila ampa siku saba DC kueleza sababu kushuka mapato

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, ametoa siku saba kwa Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Lupakisyo Kapange, kufanya tathmini ya uamuzi uliofanyika wa kuhamisha magari madogo (Mchomoko) kutoka stendi mpya (Somanda) kwenda ya zamani kama umeathiri ukusanyaji wa mapato yatokanayo na mradi huo.

Kafulila alitoa tamko hilo jana wakati alipotembelea stendi hiyo kujionea hali halisi ya stendi hiyo na kumtaka mkuu wa wilaya na wataalam wake kufanya tathmini ya kina ambayo itaonesha kama makusanyo yamepungua au yameongezeka. Alisema serikali haikusanyi hela kwa utaratibu usio na afya kwa raia na ndiyo msingi wa uamuzi wa awali wa kuhamisha magari madogo na kuyapeleka stendi ya zamani.

Alisema maamuzi yalifanywa kwa lengo la kuondoa usumbufu kwa wananchi ambao walikuwa wakisumbuliwa walipokuwa wakienda kupata huduma hiyo.

"Mkuu wa wilaya na wataalam wako nendeni mkafanye tathmini na kama itaonekana uamuzi uliofanywa haukuwa sahihi ubadilishwe, na mpaka sasa kwa haraka haraka mapato yameshuka, hivyo mje na majibu na ushawishi wa kutosha Jumatatu wiki ijayo ambao utanifanya nibadilishe uamuzi au ubaki pale pale," alisema.

Vile vile, alisema wakati uamuzi unafanyika kuhamisha magari hayo, mkuu wa wilaya na wamiliki wa magari walimhakikishia kuwa mapato ya halmashauri hayataathirika, jambo ambalo limeonekana kuwa sio kweli na kwamba uhalisia unaonesha mapato yameshuka kwa kiwango kikubwa. Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya mji wa Bariadi, Maganiko Msabi, alisema baada ya magari kuhamishwa makusanyo ya magari yamepungua kwa kuwa kabla ya uamuzi, halmashauri ilikusanya asilimia 75 ya lengo ndani ya stendi hiyo.

"Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 tulikusanya Sh. milioni 224.2 sawa na asilimia 75 hapo ni kabla ya magari madogo kuhamishwa, lakini kwa mwaka wa fedha 2021/2022 toka Julai 2021 hadi Machi 30, mwaka huu, tumekusanya Sh. milioni 112.2 sawa na asilimia 37 ya lengo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Lupakisyo Kapange, akitetea uamuzi wa awali, alisema kilichosababisha kushuka kwa mapato sio uamuzi huo bali kuna mianya ya upotevu wa mapato.

Alisema baadhi ya watu wanahujumu stendi hiyo na kusababisha kupungua kwa mapato kutokana na baadhi ya mabasi makubwa kupakia abiria nje ya stendi tofauti na utaratibu.

Baadhi ya mawakala wamempongeza Mkuu wa mkoa kwa kutembelea stendi hiyo na kumueleza kuwa uamuzi uliofanyika haukuwa sahihi kwa kuwa ndiyo chanzo cha kupungua mapato na ni vyema magari madogo yarudishwe.

# Taksi mtandao waliokiuka bei elekezi matatani

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imewapa baadhi ya wamiliki wa taksi mtandao siku saba za kutoa utetezi kutokana na kukiuka viwango elekezi vya nauli kabla haijatoa adhabu za kiudhibiti.

Hatua hiyo imekuja baada ya madereva wa taksi mtandao kuandamana katika ofisi za mamlaka hiyo jijini Dar es Salaam, wakishinikiza kusitishwa kwa leseni za wamiliki wa mifumo ya taksi hizo waliokiuka viwango vya ukomo.

Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo, Gilliard Ngewe, alikiri kuwa licha ya bei elekezi kuanza kutumika rasmi Aprili 8, mwaka huu, mpaka sasa kuna baadhi ya wamiliki wa taksi hizo hawafuati viwango elekezi vya nauli na kamisheni.

"Mamlaka ilichukua hatua kwa mujibu wa sheria na kanuni za LATRA ambapo wamiliki wa mifumo waliokiuka viwango walipewa amri ya utekelezaji (compliance order) inayowataka kutoa utetezi wao ndani ya siku saba kutokana na ukiukwaji waliofanya kabla mamlaka haijatoa adhabu za kiudhibiti," alisema na kuongeza:

"Mamlaka pia ilichukua hatua ya kufanya kikao na viongozi wa madereva hao. LATRA inapenda kusisitiza wadau wote wa usafirishaji kuzingatia sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini namba tatu ya mwaka 2019 na kanuni za huduma ya usafiri wa kukodi (private hire services) za mwaka 2020," alisisitiza Ngewe.

Mmoja wa madereva hao, Khatibu Haji, alidai kuwa wamiliki wa taksi mtandao (Uber na Bolt) hawataki kupandisha bei ya nauli kitu ambacho kinawaumiza.

"Tuliamua kwenda LATRA kwa sababu wao ndiyo waliowapa leseni Uber na Bolt, kuna wamiliki wengine wameshaongeza bei ya nauli, lakini wao hawataki, hivyo wateja hawawezi kwenda kwenye (Application) programu yenye bei kubwa.

"Tunataka LATRA wafanye maamuzi, tulifanya kikao nao, lakini tukashindwana kwa sababu wanaishia kusema wamewaandikia Uber na Bolt barua, kila siku hivyo hivyo, ndiyo maana tukaamua kuwafuata ofisini kwao watueleze vizuri," alisema Haji.

## Wataalamu Tanzania, Kenya wakagua mpaka

**Na Munir Shemweta,** WANMM SERENGETI

TIMU ya wataalamu wa mipaka kati ya Tanzania na Kenya, imetembelea na kujionea kazi ya uimarishaji mipaka wa kimataifa wa nchi hizo iliyofanywa kwa lengo la kukagua na kushauri namna bora ya kuendelea na kazi zinazofuata.

Ukaguzi wa mipaka hiyo ulifanyika jana ikiwa ni sehemu ya kikao cha pamoja cha wataalam wa mipaka wa nchi hizo kilichoanza juzi kwa ajili ya kupokea mawasilisho ya kazi iliyofanyika sambamba na kutoa mwongozo wa namna bora ya kutekeleza kazi iliyobaki.

Wataalam hao wakiongozwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Hamdouny Mansoor na Juster Nkoro, Mtendaji Mkuu, Ofisi ya Mipaka ya Kimataifa nchini Kenya (KIBO) walitembelea mpaka wa Tanzania na Kenya eneo la Kirongwe wilayani Rorya kwa upande wa Tanzania na Muhuru Bay katika Kaunti ya Migori nchini Kenya na ule wa nchi hizo eneo la Serengeti/Masai Mara ili kukagua kazi ya uwandani.

Timu ya wataalamu wa mipaka kutoka Tanzania na Kenya, tayari imekamilisha uimarishaji mpaka wa kimataifa wa nchi hizo kipande cha kilomita 83 kutoka hifadhi ya Serengeti/Masai Mara hadi Ziwa Natron na awamu ya pili ya kipande cha kilomita 110 uimarishaji wake utaendelea baada ya kukamilika kuandaliwa mpango kazi. Wakati wa ufunguzi wa kikao cha pamoja cha wataalam hao, Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Kanali Michael Mangwela, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mara, aliwaambia washiriki kuwa uimarishaji mipaka ulenge kuimarisha uhusiano na kujadili changamoto za maeneo ya mipakani.

Mwakilishi wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Kenya, Balozi Joseph Vungo, alishauri wataalamu wanaoshiriki kikao hicho kuhakikisha wanajadili na kuzitolea uamuzi changamoto kwa amani hasa wakizingatia Tanzania na Kenya zimekuwa na uhusiano mzuri.

Mpaka wa Tanzania na Kenya eneo la nchi kavu una ukubwa wa kilomita 758 na uimarishaji wake utasaidia kuondoa changamoto mbalimbali zilizokuwa zikijitokeza kutoka kwa wananchi wanaofanya shughuli maeneo ya mipakani katika nchi hizo.

# Wanachama 19 wa CHADEMA waanza kusomewa maelezo

**Na Richard Makore,** MWANZA

WANACHAMA 19 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wameanza kusomewa maelezo ya awali ya kesi yao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, huku upande wa mashtaka ukiahidi kupeleka mashahidi saba wakiwamo viongozi wa Kanisa Katoliki Parokia ya Kawekamo Jimbo Kuu la Mwanza na vielelezo vinne vya ushahidi.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na kosa la kufanya ghasia katika mkutano wa dini uliofanyika katika Kanisa hilo, Agosti 15, mwaka 2021 na kusababisha waamini washindwe kusikiliza neno la Mungu.

Kesi hiyo namba 77 ya mwaka 2021 ilifunguliwa Oktoba 19, 2021 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Mwanza na tangu wakati huo jana ndiyo washtakiwa walianza kusomewa maelezo ya awali.

Wafuasi hao ambao wapo nje kwa dhamana tangu mwaka jana, walifika tena katika mahakama hiyo, kwa ajili ya kusomewa maelezo ya awali.

Wakili wa serikali, Gisela Banturaki, alidai mahakamani kwamba siku ya tukio, wanachama hao walivaa mavazi ambayo yalisababisha waumini washindwe kusikiliza neno la Mungu na kuanza kuwaangalia.

Alidai siku ya tukio washtakiwa walikuwa wamevaa fulana zilizoandikwa neno 'Katiba Mpya' na mavazi yanayovaliwa na wanachama wa CHADEMA na walipoingia kanisani walisababisha usumbufu kwa waumini hao.

Pia, alidai baada ya kutokea usumbufu huo, viongozi wa kanisa hilo waliwaita na kuwataka watoke nje ili wakabadilishe mavazi hayo, lakini walikaidi.

Alidai baada ya kukaidi agizo la viongozi wa kanisa, waliita polisi kwa ajili ya kuwakamata.

Vile vile, alidai baada ya polisi kuwakamata wanachama hao waliwapeleka kituo kikuu cha polisi, jijini Mwanza.

Kesi hiyo ambayo ipo chini ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mkoa wa Mwanza, Bonaventure Lema, upande wa mashtaka unatarajia kupeleka mashahidi saba wakiwamo viongozi wa dini wa kanisa hilo na vielelezo vinne vya ushahidi.

Wakili wa serikali alidai mahakamani kwamba wana mashahidi saba pamoja na vielelezo na wataanza kutoa ushahidi Mei 17, mwaka huu.

Agosti 19, mwaka jana, wanachama hao wakiwamo viongozi wa mikoa ya Kanda ya Victoria, walikamatwa wakiwa kanisani kwa ajili ya kufanya misa ya kumuombea Mwenyekiti wao Taifa, Freeman Mbowe, ambaye alikuwa mahabusu kwa kesi ya ugaidi.

Washtakiwa wote walikana mashtaka yao na wanatetewa na Wakili Eric Muta.

Wakati huo huo, viongozi wa chama hicho Kanda ya Victoria, wamelalamikia simu zao pamoja na kompyuta kuendelea kushikiliwa na polisi.

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Victoria, Zakaria Obadia, akizungumza nje ya mahakama hiyo, alisema licha ya kesi yao ya awali kufutwa, polisi wamekataa kuwapatia vitu vyao.

Obadia alisema, yeye na wenzake kabla ya kesi hiyo, walikamatwa Julai 20, mwaka jana pamoja na Mwenyekiti wa CHADEMA, Mbowe kwa kosa la kutaka kufanya mkutano wa kudai Katiba mpya, jijini Mwanza bila kibali.

Alisema tangu wakati huo simu zao zimeendelea kushikiliwa na polisi licha ya Ofisi ya Mwendesha Mashtaka (DPP), kufuta kesi.

Aliomba jeshi hilo kuwapa simu zao badala ya kuendelea kuzishikilia bila sababu za msingi mpaka sasa na kwamba wamekuwa wakipigwa kalenda wanapozifuatilia.

Akizungumzia malalamiko hayo hivi karibuni, Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Khamis Mwampelwa, alisema hana taarifa kuhusu simu za viongozi hao kushikiliwa.

Alisema kama kweli zinashikiliwa, wafike ofisini kwake ili wamueleza aweze kuwasaidia kuzipata.

Hata hivyo, Obadia alisema walitikia wito huo wa kamanda na kufika ofisini kwake, lakini bado wameendelea kuzungushwa bila kupewa vifaa vyao.

## Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationship beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | | Mwaka wa sasa 31-DES-21 | Mwaka Uliopita 31-DES-20 |
|---|---|---|---|---|
| A. | | **MALI** | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 1,905 | 1,758 |
| | 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 16,405 | 13,599 |
| | 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 51,033 | 49,837 |
| | 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,663 | 3,549 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| | 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 23,972 | 18,803 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 70,515 | 69,749 |
| | 12 | Mali Nyingine | 2,548 | 2,556 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| | 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| | 15 | Kodi iliyoahirishwa | 74 | 52 |
| | 16 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 3,021 | 1,947 |
| | **17** | **JUMLA YA MALI** | **171,136** | **161,850** |
| B. | | **B. DHIMA** | | |
| | 18 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 57,932 | 53,125 |
| | 19 | Amana za Wateja | 70,619 | 68,384 |
|---|---|---|
| Dr. Edwin P. Mhede<br>**Mwenyekiti wa Bodi** | | Machi 30, 2022 |
| Benson Mahenya<br>**Mkurugenzi** | | Machi 30, 2022 |

BENKI BORA TANZANIA
TUZO 7 ZA KIMATAIFA
Asante kwa kuchagua Benki ya NMB!



# CITIBANK TANZANIA LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | 2021 TZS '000 | 2020 TZS '000 |
|---|---|---|
| Mapato ya Riba | 30,977,650 | 31,302,946 |
| Gharama za Riba | (7,738,697) | (12,191,777) |
| **Mapato Halisi ya Riba** | **23,238,953** | **19,111,169** |
| Ada na Kamisheni | 5,144,355 | 4,645,837 |
| Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 9,486,490 | 8,822,446 |
| **Jumla ya Mapato** | **37,869,798** | **32,579,452** |
| Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (558,921) | 149,649 |
| **Jumla ya Mapato baada ya Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo** | **37,310,877** | **32,729,101** |
| Mishahara na Mafao | (9,501,523) | (7,974,742) |
| Uchakavu wa Mali | (1,947,302) | (1,905,423) |
| Gharama za kiutawala | (14,539,494) | (15,479,588) |
| | **(25,988,319)** | **(25,359,753)** |
| Faida /(Hasara) ya Uendeshaji | 11,322,558 | 7,369,348 |
| Tengo la Kodi ya Mapato | (3,758,502) | (2,312,847) |
| **Faida Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **7,564,056** | **5,056,501** |
| **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | |
| – Mapato ambayo hayajakamilika | 373,260 | 231,840 |
| – Tengo la Kodi ya mapato ambayo hayajakamilika | (111,978) | (69,552) |
| **Mapato mengine baada ya kodi ya mapato** | 261,282 | **162,288** |
| **Jumla ya Faida iliyojumuishwa** | **7,825,338** | **5,218,789** |

### VIASHIRIO VYA UFANISI

| | 2021 | 2020 |
|---|---|---|
| Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Fedha za Wanahisa | 7.44% | 5.11% |
| Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Mali | 0.67% | 0.38% |
| Uwiano wa gharama na mapato | 68.63% | 77.84% |
| Uwiano wa mapato halisi ya riba kwa mali zinazozalisha | 2.48% | 1.67% |
| Uwiano wa Mapato yasiyo ya riba kwa Pato | 38.63% | 41.34% |
| Uwiano wa Mikopo kwa amana za wateja | 33.5% | 27.34% |
| Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.00% | 0.00% |
| Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 81.33% | 85.76% |
| Ongezeko la Mali | -13.69% | 53.70% |
| Ongezeko la Mikopo Halisi kwa wateja | -3.59% | 5.63% |
| Ongezeko la Amana za wateja | -21.36% | 71.06% |

### WARAKA MIZANIA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | 2021 TZS '000 | 2020 TZS '000 |
|---|---|---|
| **MALI** | | |
| Fedha Taslimu na Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 185,271,074 | 133,165,746 |
| Mikopo Halisi kwa benki | 145,185 | 674,660,811 |
| Chombo cha kifedha kinachotokana na Mali | 444,505,925 | 2,121 |
| Uwekezaji katika Amana za Serikali | 63,994 | 150,449,567 |
| Mikopo Halisi kwa wateja | 184,309,427 | 319,223,382 |
| Mali Nyingine | 307,774,460 | 38,356,233 |
| Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 13,496,236 | 9,210,251 |
| Mali ya kodi ya kampuni | 542,960 | 698,929 |
| Haki ya matumizi ya mali | 7,610,392 | 5,180,568 |
| Malipo ya kodi yanayotarajiwa baadae | 4,550,643 | 3,093,162 |
| Hundi na miamala ya Kushughulikiwa | 3,361,494 | 243,262 |
| **JUMLA YA MALI** | **1,151,631,790** | **1,334,284,032** |
| **DHIMA** | | |
| Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 93,056,490 | 904,063 |
| Amana za Wateja | 918,403,379 | 1,167,796,367 |
| Chombo cha kifedha kinachotokana na Dhima | 7,499 | 25,618 |
| Dhima Nyingine | 34,347,647 | 61,995,778 |
| Dhima ya kukodisha | 4,130,816 | 4,645,084 |
| **JUMLA YA DHIMA** | **1,049,945,831** | **1,235,366,910** |
| **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 9,659,900 | 9,659,900 |
| Akaunti Nyingine za Mtaji | 2,020,619 | 1,759,337 |
| Tengo la ziada ya jumla | 604,577 | 1,582,094 |
| Mapato Yaliyobakizwa | 89,400,863 | 85,915,791 |
| **Jumla ya fedha za wanahisa** | **101,685,959** | **98,917,122** |
| **Jumla ya fedha za wanahisa na dhima** | **1,151,631,790** | **1,334,284,032** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | 2021 TZS '000 | 2020 TZS '000 |
|---|---|---|
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Faida ya Uendeshaji | **11,322,558** | **7,369,348** |
| *Marekebisho kwa Ajili ya:* | | |
| Uchakavu wa Mali | 1,947,302 | 1,905,423 |
| Uchakavu wa haki ya matumizi ya mali | 642,444 | 640,895 |
| Faida/(hasara) ya mapato mengine yaliyojumuishwa -mali | (61,873) | 42,446 |
| Faida/(hasara) ya mapato mengine yaliyojumuishwa -dhima | (18,119) | 25,618 |
| Gharama za tengo katika mikopo | 558,921 | (23,012) |
| Mapato Halisi ya Riba | (23,238,953) | (19,111,169) |
| Faida juu ya uuzaji wa mali na vifaa | 1,051 | (29,208) |
| | **(8,846,669)** | **(9,179,659)** |
| **Mabadiliko katika shughuli za uendeshaji wa mali na madeni** | | |
| Mikopo Halisi kwa wateja | 11,192,118 | (16,971,700) |
| Amana za benki nyingine | 92,152,427 | (52,634,829) |
| Uwekezaji wa Amana za Serikali | (33,710,513) | 5,514,341 |
| Hifadhi ya chini ya kisheria | 25,844,272 | (9,333,574) |
| Mali Nyingine | 24,869,976 | (21,973,713) |
| Amana za Wateja | (249,392,988) | 485,095,659 |
| Dhima Nyingine | (32,708,939) | 25,203,007 |
| **Fedha iliyozalishwa kutokana na shughuli za uendeshaji** | **(170,600,316)** | **405,719,532** |
| Riba iliyopokelewa | 30,977,650 | 31,302,946 |
| Riba iliyolipwa | (7,738,697) | (12,191,777) |
| Kodi iliyolipwa | (3,982,843) | (2,703,497) |
| **Fedha Halisi zilizotumika kwa shughuli za uendeshaji** | **(151,344,206)** | **422,127,204** |
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji** | | |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (348,494) | (1,261,294) |
| | - | 29,208 |
| **Fedha Halisi Zilizotumika kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(348,494)** | **(1,232,086)** |
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha** | | |
| Malipo kwa ajili ya dhima ya kukodisha | (526,786) | (1,181,304) |
| Gawio lililolipwa | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotumika kwa Shughuli za Kifedha** | **(526,786)** | **(1,181,304)** |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka** | **749,305,949** | **482,484,590** |
| Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji | (151,344,206) | 422,127,204 |
| Fedha Halisi Zilizotumika kwa Shughuli za Uwekezaji | (348,494) | (1,232,086) |
| Fedha Halisi Ziilizotumika kwa Shughuli za Kifedha | (526,786) | (1,181,304) |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka** | **597,086,463** | **749,305,949** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa TZS '000 | Akaunti nyingine za mtaji TZS '000 | Mapato Yaliyobakizwa TZS '000 | Tengo la ziada ya kisheria TZS '000 | Jumla TZS '000 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 1 Januari 2021** | **9,659,900** | **1,759,337** | **85,915,791** | **1,582,094** | **98,917,122** |
| Faida Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 7,564,056 | - | 7,564,056 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | 261,282 | - | - | 261,282 |
| **Jumla ya Faida iliyojumuishwa kwa mwaka** | - | 261,282 | 7,564,056 | - | 7,825,338 |
| Gawio litakalolipwa | - | - | (5,056,501) | - | (5,056,501) |
| Hamisho la Tengo la Ziada | - | - | 977,517 | (977,517) | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31 Desemba 2021** | **9,659,900** | **2,020,619** | **89,400,863** | **604,577** | **101,685,959** |

| | Mtaji wa Hisa TZS '000 | Akaunti nyingine za mtaji TZS '000 | Mapato Yaliyobakizwa TZS '000 | Tengo la ziada ya kisheria TZS '000 | Jumla TZS '000 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 1 Januari 2020** | 9,659,900 | 1,597,049 | 92,611,318 | - | 103,868,267 |
| Faida Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 5,056,501 | - | 5,056,501 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | 162,288 | - | - | 162,288 |
| **Jumla ya Faida iliyojumuishwa kwa mwaka** | **-** | **162,288** | **5,056,501** | **-** | **5,218,789** |
| Gawio lililolipwa | - | - | (10,169,934) | - | (10,169,934) |
| Hamisho la Tengo la Ziada | - | - | (1,582,094) | 1,582,094 | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31 Desemba 2020** | **9,659,900** | **1,759,337** | **85,915,791** | **1,582,094** | **98,917,122** |

Taarifa hizi zilipitishwa na Bodi ya Wakarugenzi tarehe 31 Machi 2022 na kutiwa saini kwa niaba yake na::

Geofrey Mchangila
**Ofisa Mtendaji Mkuu**

Andulile Mwakalyelye
**Mjumbe wa Bodi**

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2014, na zinaonesha hali halisi.

Godwin Rutashobya
**Mkaguzi Mkuu wa Ndani**

Wilson Chola
**Mjumbe wa Bodi**

Andulile Mwakalyelye
**Mjumbe wa Bodi**





# Wito dini, sekta binafsi kubana watakaokwaza mchakato sensa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIONGOZI wa taasisi za kidini na sekta binafsi mkoani Dodoma, wameshauriwa kuzikemea jamii zitakazokwamisha uandikishaji wa sensa ya watu na makazi.

Aidha viongozi hao pia wameshauriwa kutoa elimu ya kina ili jamii hizo zenye malengo ya kupotosha zoezi hilo ziweze kushiriki kikamilifu na kujitokeza ili kuhesabiwa na serikali kufikia malengo yake.

Rai hiyo ilitolewa kwa nyakati tofauti na viongozi hao walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari kwa lengo la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan ambaye hivi karibuni alizindua nembo ya sensa hiyo mjini Zanzibar.

Rais alizindua nembo ya sensa na kutangaza rasmi kuwa itaanza Agosti 23, mwaka huu, huku akisisitiza kuwa elimu zaidi itolewe ili kufanikisha jambo hilo.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande, alisema sensa ya watu na makazi siyo mkosi au laana, hivyo viongozi wanatakiwa kuisaidia serikali katika kuelimisha jamii ambayo bado wanaamini kuwa suala hilo lipo kiimani zaidi.

Wakielimishwa pamoja na kukemewa serikali itafikia malengo yake kwa kuwa hata wenye imani potofu watajitokeza kwa wingi kwa uaminifu na kuweza kuhesabiwa.

Dk. Chande alisema Watanzania wote bila kujali itikadi yoyote, wanatakiwa kuisadia serikali badala ya kuipinga, ili mpango wa kujua mahitaji kulingana na idadi ya watu wake ufanikiwe.

Alisema kuwa kama inavyofanyika kwa upande wa UVIKO-19 katika kuhakikisha watu wanajitokeza kupata chanjo,pia kwenye zoezi la sensa ya watu na makazi nalo wahakikishe wanajitokeza ili wahesabiwe kila mmoja.

Fundi Mkuu wa Karakana ya Walemavu Dodoma (KAWADO), Mwita Marwa, aliwataka viongozi kubadili mtazamo wa jamii katika masuala ya sensa.

Pai alizionya familia zenye watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali kutowanyima fursa ya kuandikishwa kwenye zoezi hili la sensa.

Mwenyekiti wa wanawake wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Jimbo la Dodoma, Shile Sheshu, aliwaomba wanawake kumuunga mkono Rais Samia kwa kujitokeza na kutoa majibu sahihi kwenye zoezi hilo la uandikishaji wa watu na makazi.

Alisema kuwa wanawake wengi ndiyo wanaokaa na familia, hivyo wanatakiwa kushiriki kwa kuumunga mkono Rais ili serikali iweze kupata idadi kamili inayohitaji kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

"Sensa ni kitu muhimu sana kwa Watanzania, hivyo tusiwe waoga wa kujibu na kutoa takwimu sahihi ya watu tunaoishi nao kwenye familia zetu, wote hao wanatakiwa kuhesabiwa bila kujali kuna vikongwe na walemavu,"alisema.

# Mwongozo kuwabana watoa huduma msaada wa saikolojia wasio na weledi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imepitisha na kusambaza mwongozo wa kitaifa wa utoaji wa huduma ya msaada wa akili na kisaikolojia utakao wabana watoa huduma hizo wasiokuwa na weledi wa kutosha.

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwajuma Magwiza, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao cha kupitisha na kusambaza mwongozo wa kitaifa wa utoaji wa huduma ya msaada wa akili na kisaikolojia.

Magwiza, alisema pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali, huduma hizo zinatolewa na watoa huduma wasio na weledi wa kutosha katika eneo hilo na bila utaratibu.

"Mwongozo huu wa kitaifa na taratibu hizi zimeandaliwa kwa lengo la kuwaelekeza na kuwawezesha watoa huduma kutoa msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa utaratibu, ubora na uendelevu katika ngazi ya mtu mmoja mmoja, familia na jamii kwa ujumla.

"Serikali inatambua kuwa utekelezaji wa taratibu hizi unahitaji ushirikiano na kuhusisha watendaji na wadau mbalimbali katika kushughulikia mahitaji ya kisaikolojia na kijamii," alisema.

Alisema kipekee anawashukuru Shirika la Umoja wa Mataifa International Organization for Migration (IOM) kudhamini, kupitisha na kusambaza mwongozo huo na kuwezesha waalikwa kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara kufika kwenye kikao hicho.

Magwiza alisema Tanzania inakabiliana na changamoto za kijamii na kiuchumi zinazotokana na umaskini, kudhoofika kwa mifumo ya jadi ya hifadhi ya jamii, maafa, ukosefu wa ajira, magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama saratani, kisukari na shinikizo la damu.

Aidha, alisema changamoto hizo zimeathiri kwa kiasi kikubwa ustawi wa kisaikolojia na kijamii kwa mtu mmoja mmoja, familia, kaya na jamii kwa ujumla.

Alibainisha kuwa maendeleo makubwa yamefanyika nchini kutokana na sera na misingi ya kisheria ili kukabiliana na changamoto hizo.

"Sera na misingi hiyo ya kisheria ni pamoja na Sera ya Taifa ya Afya ya 2007, Sera ya Taifa ya Wazee ya 2003, Sera ya Taifa ya Watu wenye ulemavu ya 2004, Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya 2008, Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu ya 2008, Sheria ya Mtoto ya 2009, Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya 2010, na Mpango wa kuzuia na kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto 2017-2022," alisema.



Meneja wa Kiwanda cha Serengeti Breweries Ltd (SBL) Moshi, Alice Kilembe (wa pili kulia), akikabidhi blanketi kwa mmoja wa wazee wa Mwika, wakati SBL ilipotoa msaada wa mablanketi 150 kwa wazee hao, katika Kata ya Mwika, mkoani Kilimanjaro mapema wiki hii. Kulia ni Mjumbe wa kamati ya Klabu ya Mwika Rotary wanaoratibu huduma za wazee hao katika kata hiyo, Ester Towo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampeni ya TAKUKURU yafikia wakazi 86%

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoani Dodoma, imefikia asilimia 86 ya wakazi wa jijini hapa, katika kampeni ya Ulipo Twaja iliojikita kutoa elimu ya kupinga rushwa kwa wananchi kwenye maeneo yao ya kazi.

Taarifa iliyotolewa na Mkuu wa TAKUKURU mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, inasema kuwa kampeni hiyo imechangia kuongeza idadi ya taarifa ambazo taasisi hiyo inazipokea kwa njia ya simu kuhusu rushwa ikiwemo ukiukwaji wa maadili.

Alifafanua kuwa TAKUKURU Dodoma inaamini kupanda mbegu ya mabadiliko katika mioyo ya wakazi wa Dodoma ni moja ya utekelezaji wa wajibu wao kwa kuzuia vitendo vya rushwa.

"Kampeni ya Ulipo Twaja imekamilishwa mwishoni mwa Machi mwaka huu na imefanikiwa kwa kiasi kikubwa na kuleta matokeo chanya," alisema Kibwengo.

Kibwengo alitaja baadhi ya maeneo ambayo kampeni ya Ulipo Twaja imefika ni pamoja na kwa wachuuzi wa samaki wanaokusanyika soko la Bonanza Jijini Dodoma,Mpunguzi, Hombolo, Kibaigwa, Mundemu, Handali, Cheku, Kidoka, Makanda, Songambele, Mpwayungu, Hamia, Mlowa-barabarani, Veyula, Haneti.

Alisema maeneo mengine ni Mbabala, Kizota, Paranga, Mbande, Tambi, Gwandi, Mkonze, Kibakwe, Msisi, Buigiri, Mvumi, Mbande, Babayu, Mrijo, Chase, Soera, Kwantisi, Mayamaya, na maeneo mengine mengi nao walifikiwa.

Alisema katika maeneo hayo timu ya wataalamu ilifanya uelimishaji kwa kutumia mbinu na nyenzo mbalimbali ikiwemo kutia mkazo mkubwa wa kazi hii ya kukuza ufahamu, utayari na uthubutu wa kuwa majemedari wa mapambano dhidi ya rushwa ili kuhakikisha kuwa mkakati maalum unawekwa katika kuwafikia watu wengi wa rika la chini hadi wakubwa.

Aliongeza kuwa kuna kundi kubwa la wanajamii ambalo kwa aina ya shughuli zao za kila siku sio rahisi kupata fursa ya kushiriki katika mikutano ya hadhara, hivyo maonyesho na mikusanyiko mingine rasmi inayoandaliwa na taasisi hiyo kwa ajili ya kuelimishwa, iliona ni vema kuandaa utaratibu maalum wa kuwafuata wananchi hao walipo katika mikusanyiko.

"Ni matarajio ya TAKUKURU kwamba, baada ya elimu, masikio ya waelimishaji na macho kwa kusoma vipeperushi walivyogawiwa, yatakuwa viungo muhimu vya kukoleza chachu ya mabadiliko ya kutoifumbia macho rushwa,"alisema Kibwengo.

Aliongeza kuwa kampeni hiyo pia iliwafikia wauzaji na wanunuzi wa bidhaa sokoni, minadani na magulioni ambapo walielimishwa.

Pia, kero zao kusikilizwa katika wilaya ya Bahi ambapo vijana wa bodaboda katika vijiwe vyao walifikiwa,wafanyabiashara,wasafiri na wasafirishaji waliokusanyika katika minada mbalimbali Jijini Dodoma.





# Mbarali sasa wakumbukwa kwa kujengewa barabara

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

SERIKALI imetoa Sh. milioni 204 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Igalako- Mwatenga hadi Kilambo ambayo tangu uhuru haijawahi kufanyiwa maboresho.

Barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 21 imeanza kutengenezwa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya ambayo kwa kushirikiana na mkandarasi wa mradi huo MS/ Ubaruku Limited wanaendelea na shughuli za ujenzi.

Akizungumza jana wakati wa ziara ya kukagua matengenezo ya barabara hiyo, ikiongozwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, Meneja wa TARURA wilayani humo, Mhandisi Rashid Kavandama, alisema hadi sasa ujenzi wa barabara hiyo umefikia asilimia 30.

Alisema fedha za mradi huo, zimetokana na makusanyo ya tozo za miamala ya simu kupitia mfuko wa barabara ambapo Oktoba 31 mwaka 2021 mradi huo ulianza kutekelezwa lakini kutokana na kunyesha kwa mvua za masika ilichangia kupunguza kasi ya matengenezo ya barabara hiyo.

Alisema makubaliano ya ujenzi wa barabara hiyo ni kwamba hadi kufikia Juni 29, mwaka huu barabara hiyo itakuwa imekamilika na wananchi wataendelea kuitumia kwa ajili ya shughuli zao za uzalishaji mali kama vile kusafirisha mazao kutoka shambani hadi kwenye makazi yao.

" Mradi huu unatekelezwa na TARURA kupitia mfuko wa barabara unaotokana na tozo za miamala ya simu ya shilingi milioni 204 tuliopatiwa na serikali kujenga barabara hiyo ambayo imekuwa korofi kwa kipindi kirefu, mkandarasi yuko saiti anaendelea na kazi na sisi Tarura tunaendelea kukagua na kufuatilia kila hatua za marekebisho ya barabara hii," alisema Mhandisi Kavandama.

Aliongeza kuwa kazi inayoendelea kwa sasa ni kuendelea kuinua tuta la barabara kilomita tatu ili kuzuia barabara hiyo kumomonyoko na kuharibiwa na mvua au mifereji ya maji inayoingia kwenye mashamba ya mpunga.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kilambo, Mwakami Matiga, aliishukuru serikali kwa kuwatengenezea barabara hiyo na kwamba tangu enzi za ukoloni barabara hiyo haijawahi kufanyiwa marekebisho.

Alisema kipindi cha masika mawasiliano ya barabara hiyo yalikuwa yanakatika na kukwamisha shughuli zote za kiuchumi ikiwamo kilimo cha mpunga, ufugaji na watoto kwenda shule.

Aliongeza kuwa kukamilika kwa barabara hiyo kutachochea maendeleo kwani wakulima watasafirisha mazao yao bila vikwazo, wananchi kupata huduma za kijamii kwa wakati.

Akikagua maendeleo ya mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alimtaka mkandarasi anayesimamia mradi huo kujenga kwa kuzingatia viwango vinavyohitajika.

Aidha aliitaka TARURA kuendelea kufuatilia na kuhakikisha matengenezo ya barabara hiyo yanakamilika kwa wakati uliopangwa kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia fedha hizo kukamilisha ujenzi wa barabara ambayo kwa kipindi kirefu haikufanyiwa marekebisho na kurahisisha shughuli za usafiri kwa wakazi wa Kata ya Mwatenga.



Mwenyekiti wa Kijiji cha Kilambo, Kata ya Mwatenga, wilayani Mbarali, mkoani Mbeya, Mwatami Matiga (katikati), akifafanua jambo kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune (kulia), alipotembelea kukagua ujenzi wa barabara ya Igalako-Mwatenga-Kilambo yenye urefu wa kilomita 21, juzi, akiwa na kamati ya ulinzi na usalama. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wataalamu afya ya meno, kinywa waonywa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WATAALAMU wa afya ya kinywa na meno nchini, wametakiwa kuacha kuziba meno bila kutumia dawa yenye madini ya zebaki (Amalgma).

Ushauri huo umetolewa baada ya kubainika kuwa na athari za kiafya kwa binadamu.

Wito huo ulitolewa jana na ofisa kutoka Idara ya Tiba ya kinywa na meno kutoka Wizara ya Afya, Dk. Msafiri Kabulwa, wakati wa mafunzo kwa wataalamu wa afya ya kinywa na meno kuhusu kuziba meno kwa kutumia kemikali zisizo na madini ya zebaki yaliyofanyika jijini Mbeya.

Dk. Kabulwa alisema madini ya zebaki yana athari katika afya ya binadamu kwani inaharibu ukuaji wa ubongo wa mtoto tangu akiwa tumboni kwa mama yake.

"Nawashauri watoa huduma wenzangu kuacha matumizi ya zebaki kwenye afya ya kinywa na meno kwa sababu madini hayo huweza kutoka kwa mama mjamzito na kuingia kwa mtoto aliye tumboni wakati wa ujauzito, ama kupitia maziwa ya mama wakati wa kunyonyesha na kuleta athari katika ukuaji wa ubongo wa mtoto," alisema Dk. Msafiri.

Alieleza athari nyingine zitokanazo na matumizi hayo ya zebaki kuwa ni kuharibu uwezo wa mtoto wa kufikiri na hatimae kumfanya mtoto kushindwa kulitumikia taifa lake vyema.

Katika kuhakikisha Wizara ya Afya inaendelea kutoa elimu ya afya ya kinywa na meno kwa wataalamu wa afya na wananchi, Msafiri alisema wizara imelenga kuikinga jamii dhidi ya madhara yatokanayo na madini ya zebaki kwa kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kuzibia meno zisizokuwa na madini ya zebaki kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

Alihamasisha matumizi ya kemikali za kuzibia meno zisizokuwa na madini ya zebaki kuwa zinapatikana hapa nchini kwa wasambazaji binafsi na kupitia MSD.

Ofisa Programu Mwandamizi wa Asasi ya AGENDA, Dorah Swai, alisema mwaka 2013 Tanzania iliungana na nchi nyingine ulimwenguni kusaini mkataba wa kimataifa wenye lengo la kulinda afya na mazingira kutokana na athari za zebaki.

Mkataba huo unaojulikana kama Minamata wa zebaki uliridhiwa na Tanzania Oktoba 2019 na kuongeza kasi ya utekelezaji wake kwa kuzingatia miongozo na kanuni.

## Kibano chaja ucheleweshaji anwani makazi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, amewataka watendaji wa kata, wenyeviti wa vijiji na vitongoji kuhakikisha wanakamilisha mchakato wa anwani za makazi kabla ya Aprili 30, mwaka huu na kuahidi kuwachukulia hatua za kisheria watakao kwamisha.

Mfune alitoa kauli hiyo jana kwenye mkutano wa hadhara alioufanya katika Kata ya Ihahi na Itamboleo ambapo alitumia nafasi hiyo kuwataka watendaji wa vijiji na kata kuhakikisha zoezi hilo linakamilika kabla ya Aprili 30, mwaka huu, na kwamba maeneo yote muhimu yaliyotengwa na wananchi yafikiwe.

Alisema lazima kila mwananchi ashiriki kwenye zoezi hilo la anwani za makazi kwa maelezo kuwa linagusa moja kwa moja maisha ya Watanzania kujua idadi yao ili rasimali zitakazopatikana zitolewe kulingana na wananchi waliopo.

Alisema kukamilika kwa zoezi hilo kutarahisisha shughuli za sensa ya watu na makazi ifikapo Agosti mwaka huu.

"Nawashukuru sana wananchi kwa muitikio wenu kushiriki zoezi hilo inaonyesha ni jinsi gani mnatamani kupata maendeleo, nimeona vijiji na vitongoji vyenu vimepambwa na vibao vya anuani za makazi, sasa kazi kwenu watendaji wa serikali za mitaa kuhakikisha maeneo yote yaliyotengwa kufikiwa na zoezi hili yanakamilika mtendaji atakayekwamisha atashughulikiwa," alisema Mfune.

Mwenyekiti wa kijiji cha Itamboleo, Samwel Kaganga, alisema hadi kufikia April 20 mwaka huu zoezi la anuani za makazi katika eneo lake litakuwa limekamilika.

Aidha, aliwaomba wananchi wa eneo hilo kuendelea kuchangia sh. 1000 kama gharama ya utengenezaji wa vibao hivyo ambayo vitawekwa kwenye makazi ya watu.

Diwani wa Kata ya Ihahi, Bahati Salum, alisema zoezi la kuweka vibao vya mitaa na namba za nyumba lilikuwa shirikishi ambapo kupitia mkutano wa hadhara wananchi walipewa nafasi ya kuchagua majina yatakayowekwa kwenye vibao hivyo.



## HABARI ZANZIBAR

# Serikali yaanza kutoa vifaa vya uvuvi

**Na Mwandishi Wetu** PEMBA

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema sio wakati wa wavuvi kulalamikia ukosefu wa vifaa na mitaji kwa sababu serikali kwa kushirikiana na wadau imeshaanza kutekeleza azma ya kuimarisha uchumi wa buluu kwa kutoa vifaa vya uvuvi.

Aliyasema hayo katika Bandari ya Shumba Mjini, Wilaya ya Micheweni Pemba, katika hafla ya ugawaji wa boti za uvuvi na mashine zake zilizotolewa na Benki ya Amana pamoja na hundi ya Sh. milioni 192 iliyotolewa na Benki ya CRDB kwa ushirika wa uvuvi wa Kijiji cha Tumbe, ikiwa ni utekelezaji wa sera ya uchumi wa buluu na ahadi yake hiyo aliyoitoa.

Alisema pamoja na vifaa hivyo, ziko benki mbalimbali na mashirika mengine kama ZAFICO zilizotenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na mitaji ambayo itatolewa kwa wavuvi ili kufikia safari yenye lengo la kuwabadilisha kimaisha.

Alitoa mfano wa benki hizo ikiwamo ya Amana iliyotenga Sh. bilion 10, Wizara ya Uchumi wa Buluu, Sh. bilioni 36, Benki ya CRDB iliyotenga Sh. bilioni 31 na Kampuni ya ZAFICO iliyotenga Sh. bilioni 7.6.

"Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendelea kushirikiana na wahisani mbalimbali zikiwamo benki ili kuwajengea mbinu za maendeleo wananchi kwa kuwapatia nyenzo mbalimbali za kujikwamua na umaskini," alisema.

Dk. Mwinyi alisema kazi ya utoaji wa boti na vifaa vyake ni miongoni mwa kufikia safari ya ajira 300,000 zilizotangazwa na serikali ambazo miongoni mwake zitatoka katika sekta mbalimbali ikiwamo ya uvuvi.

Alisema kuna haja kwa benki ambazo zimeshatenga fedha kwa ajili ya kuwezesha wananchi kufanya hivyo ili kuwasaidia wananchi wengine ambao bado hawajapatiwa vifaa vya uvuvi ili kuungana na wenzao katika safari hiyo ya kutumia rasilimali zitokanazo na bahari na kufaidika na sera ya uchumi wa buluu.

Pia, alisema ni azma ya serikali kuirasimisha bandari hiyo ya Shumba Mjini ili kufanya shughuli zake vizuri na kutoa faida zaidi kwa wananchi.

Aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha wananchi wanapewa fedha kutoka Benki ya CRDB na Benki ya Amana kwa ajili ya shughuli zao za uvuvi kama ilivyokusudiwa na kupangwa na serikali.

Alisema hatua na ushirikiano atakaoutoa katika kuhakikisha ZAFICO inaimarika, kuvua na kununua samaki, kusarifu kwa kujenga viwanda ikiwa ni utekelezaji wa uchumi wa buluu.

Alisema pia, kutatolewa boti 577 za uvuvi, kujengwa kwa viwanda vya kusarifu samaki na mwani huko kisiwani Pemba.

Akitoa maelezo, Mkurugenzi Mwendeshaji wa ZAFIKO, Dk. Ameir Haidar Mshenga, alisema mashine 16 za boti ni kwa ajili ya wavuvi wa Shumba Mjini na boti ni kwa ajili ya wavuvi wa Makangale na Kengeja ikiwa ni mwendelezo wa kutimiza ahadi aliyoitoa Dk. Mwinyi mwishoni mwa mwaka jana.

Alisema kuwa hatua hiyo inatokana na mazungumzo waliyoyafanya kati yao na Benki ya Amana kupitia Shirika la Misaada la Marekani (USAID), ambayo hatimaye yamezaa matunda, pamoja na kufanya mazungumzo na Mfuko wa Hifadhi ya jamii Zanzibar (ZSSF) ili kuwasajili wavuvi hao kwenye mfuko wa hiari kwa lengo la kujiwekea akiba.

Alisema kuwa ZAFICO imejipanga kutoa mashine za boti kwa wavuvi 650 na kuwapatia boti na mitego wavuvi 887 kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia sasa na tayari imeshaanza mazungumzo ya kuwapatia mashine 20 za boti wavuvi wa Tumbe kupitia mpango huo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Amana, Abubakar Athman Ali, alisema kuwa benki hiyo imechukua hatua hiyo ya kutoa vifaa hivyo ikiwa na azma ya kumuunga mkono Dk. Mwinyi katika kuimarisha uchumi wa buluu.

Wakati huo huo, Dk. Mwinyi, aligawa sadaka ya futari kwa wenye mahitaji maalum Micheweni wakiwamo yatima, wajane na watu wenye ulemavu.




Mkurugenzi wa Biashara wa kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Ajay Goyal (wa sita kushoto waliosimama), akiwa katika picha ya pamoja na mawakala wa usambazaji wa magazeti ya kampuni hiyo, baada ya kuzungumza nao, mjini Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Abdulla aagiza wizara kumlipa mkandarasi ujenzi hospitali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameiagiza Wizara ya Afya kuhakikisha Mkandarasi anayejenga Hospitali ya Mkoa wa Mjini iliyopo Lumumba analipwa fedha zake ili kuendelea na ujenzi wa hospitali hiyo.

Hemed aliyasema hayo wakati akiendelea na ziara ya kukagua miradi ya maendeleo inayojengwa kwa fedha za mkopo wa kukabiliana na athari za UVIKO-19.

Alisema mkandarasi wa hospitali hiyo anafanya kazi nzuri na ya kuridhisha na kwamba hafurahishwi kuona mkandarasi huyo ameshafanya maombi ya fedha kwa muda mrefu bila ya kupatiwa fedha hizo wakati serikali imeshatenga fedha zote za miradi.

Alisema kuwa serikali imeshatoa maelekezo kwa watendaji wa wizara husika zilizonufaika na miradi hiyo kuhakikisha fedha zinapatikana kwa mujibu wa mikataba na kuwataka watendaji kuwa tayari kuendana na makubaliano ya mikataba hiyo.

Katika ziara yake hiyo, aliwataka watendaji wa wizara mbalimbali kuacha tabia zisizo na msingi ambazo zinazorotesha utendaji katika serikali akitoa mfano fitina na chuki walizonazo baadhi ya watendaji serikalini.

Alisema serikali imeamua kusogeza huduma za afya karibu na makazi ili kuondoa changamoto zinazowakabili wananchi wake.

Alisema kuna watendaji wazito katika suala la malipo na kuwataka kubadilika ili kuendana na kasi ya serikali.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana Mustafa, ameishukuru serikali kwa kuona umuhimu wa kujenga hospitali kubwa ya mkoa ambayo itapunguza changamoto ya hospitali katika mkoa huo.

Alisema kuwa watasimamia ujenzi kwa mujibu wa maelekezo waliyopewa na viongozi ili kumaliza changamoto zilizopo katika miradi hiyo.

Katika ziara hiyo Makamu wa Pili, alitembelea ujenzi wa maeneo ya wafanyabiashara wadogo na ujenzi wa shule za ghorofa zilizopo ndani ya Wilaya ya Mjini Unguja na kueleza kuwa ujenzi wa maeneo hayo utapunguza changamoto zote za wafanyabiashara na wanafunzi waliopo ndani ya wilaya hiyo.

# Wanawake wahamasishwa kugombea nafasi za uongozi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKATI baadhi ya vyama vya siasa vikijiandaa na uchaguzi wa ndani wa vyama, Mkurugenzi wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar), Dk. Mzuri Issa, amewataka wanawake kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi na kutowaachia wanaume pekee nafasi hizo.

Alisema ni muhimu wanawake washike nafasi za uongozi, lakini wanapaswa kujipanga tangu mchakato wa nafasi za awali badala ya kusubiri kugombea nafasi za ubunge na uwakilishi huku wakijisahau kuwa walishindwa kujipanga awali na kutengeneza mtaji wa kura za mwanzoni.

Kauli hiyo ya Dk Mzuri imekuja siku chache baada ya Chama cha Mapinduzi (CCM) pamoja na ACT- Wazalendo kutangaza uchaguzi wa kuwania nafasi mbalimbali ndani ya vyama hivyo.

Akizungumza na waandishi wa habari Mjini Zanzibar, alisema ili wanawake wengi washike nafasi za juu za uongozi, hawana budi kujiimarisha mapema ikiwamo kugombea nafasi za matawi na majimbo kwa kuwa ndiyo kwenye mtaji mkubwa wa wapiga kura na kuacha kusubiri kugombea nafasi za juu huku wakiwa sio watu wenye kujulikana na wanachama wenzao wala ngazi zingine za vyama wanavyogombea.

"Ni lazima wanawake wafahamu kuwa uongozi hauji kama bahati ni nadra sana, lakini wanachopaswa kufanya ni kujipanga mapema ikiwamo kujitokeza kwa wingi hivi sasa kwenye chaguzi hizi za vyama vyao," alisema.

Hata hivyo, alisema inawezekana baadhi ya watu kwa malengo yao wakajitokeza kukatisha tamaa wanawake watakao jitokeza kugombea nafasi hizo jambo alilosema halipaswi kupewa nafasi na kuwataka viongozi wa vyama vya siasa kutoa fursa sawa kwa wananchama wao wote bila ya ubaguzi wa kijinsia.

Alisema asasi za kiraia kwa kushirikiana na Ubalozi wa Norway nchini, wamefanya kazi kubwa ya uhamasishaji na kuwafikia wananchi 6,917 ambao kati yao wanawake ni 4,797 na wanaume 2,120 katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba na kuna mafanikio makubwa ikiwamo uhamasishaji wa wanawake kugombea nafasi za uongozi na wanaume kuwaunga mkono.

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

UBA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 2021

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-21 | Mwaka uliopita 31-Dec-20 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,150 | 3,157 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 5,692 | 3,760 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 28,671 | 41,308 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 10,144 | 1,119 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 36,033 | 42,364 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 71,708 | 34,677 |
| 12 | Mali Nyingine | 18,899 | 4,146 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,714 | 1,203 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **178,011** | **131,734** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 25,469 | 23,878 |
| 18 | Amana za Wateja | 113,060 | 105,050 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 6,644 | 8,203 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 19 | 19 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 5,036 | 7,271 |
| 27 | Dhima Nyingine | 3,297 | 3,608 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **153,525** | **148,029** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **24,485** | **23,471** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 487 | - |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (37,540) | (40,498) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,015 | 3,445 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **24,485** | **23,471** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 945,310 | 860,148 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 4,228 | 4,102 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 579 | 225 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 13.8% | 13.7% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.9% | 7.3% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 59.9% | 49.4% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 40.3% | 32.6% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 76.6% | 82.3% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 5.7% | -5.0% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 3.8% | -24.3% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-21 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dec-20 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 12,385 | 13,516 |
| 2 | Gharama za Riba | (4,053) | (4,259) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **8,291** | **9,092** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (41) | (165) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **8,855** | **9,075** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,123 | 1,428 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 7,709 | 7,604 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 23 | 43 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(15,738)** | **(14,630)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (6,782) | (6,573) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (1,032) | (1,155) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (7,924) | (6,902) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,409** | **3,537** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (394) | (92) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,015** | **3,445** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | | |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1,015** | **3,445** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 128 | 114 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.16 | 0.55 |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 7 | 5 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| | (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.81% | 2.06% |
| | (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 5.88% | 15.07% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 74.10% | 64.76% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 0.73% | 2.44% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Limbikizo la Mwaka ya sasa 31-Dec-21 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dec-20 |
|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **1,409** | **3,445** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| - Hasara Katika Mali | 41 | 113 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo iliyoharibika | 1,611 | 329 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| - Mabadiliko Halisi ya riba | (5) | (1) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (122) | 222 |
| - hasara ya mabadilisho ya mkopo | - | - |
| - Kodi Iliyolipwa | (49) | (2,335) |
| - hasara ya mabadilisho ya mtaji | | |
| **II. Mabadiliko ya mtaji wa kazi** | | |
| - Badiliko Halisi Katika amana iliyobakizwa | (6,188) | (925) |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (7,500) | 1,329 |
| - Badiliko Halisi Katika amana ya serikali | (54,371) | (7,429) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (2,548) | (582) |
| - Badiliko Halisi Katika amana ya bank zingine | 8,378 | - |
| - Badiliko Halisi Katika amana ya mteja | 65,775 | 16,013 |
| -Riba iliyopokewa | | |
| -Riba iliyolipwa | - | - |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 423 | 949 |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **7,162** | **7,020** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (12) | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | (730) | 9 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 5 | (536) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | 9 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(737)** | **(518)** |
| ***IV. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (1,454) | (869) |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (6,846) | (6,807) |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **(8,300)** | **(7,676)** |
| V. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(1,875)** | **(1,184)** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka | 13,884 | 15,068 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka | **12,009** | **13,884** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2021** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (37,053) | - | - | - | 23,471 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 1,015 | - | - | - | 1,015 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | (487) | 487 | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(36,526)** | **487** | - | - | **24,485** |
| **Mwaka uliopita 2020** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (40,498) | - | - | - | 20,026 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 3,445 | - | - | - | 3,445 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(37,053)** | - | - | - | **23,471** |

| | *Jina na Cheo* | *Saini* | |
|---|---|---|---|
| 1 | 1 .Olugbenga Makinde<br>**Ofisa Mtendaji Mkuu** | *Imesainiwa* | *30th March, 2022* |
| 2 | Chomete Hussein<br>**Mkuu wa Fedha** | *Imesainiwa* | *30th March, 2022* |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | *Imesainiwa* | *30th March, 2022* |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| | *Jina na Cheo* | *Saini* | |
|---|---|---|---|
| 1 | 1. Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | *Imesainiwa* | *30th March, 2022* |
| 2 | 2.Oliver Alawuba<br>**Mkurugenzi** | *Imesainiwa* | *30th March, 2022* |






United Bank For Africa ( Tanzania ) Limited is a subsidiary of United Bank for Africa Plc, one of Africa's leading financial institutions offering universal banking to more than 7 million customers across 750 brances in Africa , USA and Europe .

Africa
- Tanzania
- Burkina
- Cameroon
- Chad
- Congo Brazzaville
- Congo DRC
- Côte d'Ivoire
- Gabon
- Ghana
- Guinea
- Kenya
- Liberia
- Mali
- Mozambique
- Senegal
- Sierra Leone
- Benin
- Uganda
- Zambia

Europe
UK
France

USA
New York

**TANGAZO**

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

UBA

## UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED
## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES

| S/N | ITEM/TRANSACTION | | |
|---|---|---|---|
| SECTION / | SAVINGS ACCOUNTS | RETAIL | CORPORATE |
| 1 | FREEDOM SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 15,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | 1,000 instant charge | |
| 2 | GENERAL SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| 3 | EMPLOYEE SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS15,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 USD 10 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 4 | SAVINGS ACCOUNT INDIVIDUALS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 5 | SAVINGS ACCOUNT SALARY | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 6 | SAVINGS ACCOUNT DOMICILARY | | |
| | Required minimum opening balance | USD10 | |
| | Minimum operating balance | USD 5 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | 1% per Transaction | |
| 7 | U-CARE CHILDREN SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | USD 15 | |
| | Minimum operating balance | USD 15 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 or its equivalent | |
| 8 | MALAIKA ACCOUNT | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 | |
| | Minimum operating balance | NIL | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| 9 | JANJA ACCOUNT | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 | |
| | Minimum operating balance | NIL | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| 10 | KIZAZI KIPYA ACCOUNT | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS20,000 | |
| | Minimum operating balance | NIL | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| 11 | HAZINA ACCOUNT | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS20,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS20,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| SECTION I | CURRENT ACCOUNTS | | |
| 1 | INDIVIDUAL CURRENT ACCOUNT | | BUSINESS CURRENT ACCOUNT |
| | Required minimum opening balance | TZS 30,000 | TZS 100,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 10,000 | TZS 100,000 |
| | Monthly maintenance fee | TZS 10,000 | TZS 12,000 |
| | Cash withdrawal at counter | 1 PER MILLE | TZS A/C 1 PER MILLE |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 5% | TZS A/C PLR + 10% |
| 2 | DIPLOMAT ACCOUNTS | | |
| | Required minimum opening balance | USD 100 | N/A |
| | Minimum operating balance | USD 100 | N/A |
| | Monthly maintenance fee | NIL | N/A |
| | Cash withdrawal at counter | NIL | N/A |
| | Closing account | NIL | N/A |
| | Penalty for overdrawn account | NIL | N/A |
| | Outward fund transfers(TTs) | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 200 | N/A |
| | Inward fund transfers(TTs Incoming) | NIL | N/A |
| | FOREX exchange | Favourable rates will be applied | N/A |
| 3 | DOMICILIARY CURRENT ACCOUNT | | |
| | Required minimum opening balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Minimum operating balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Monthly maintenance fee | USD 12 or its equivalent | USD 15 or its equivalent |
| | Minimum search fees | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 |
| | Cash withdrawal | 1% per Transaction | 1% per Transaction |
| | Cheque book - 25 LEAF | USD 10 or its equivalent | N/A |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 2% | PLR + 2% |
| | Transfer From TZS to DOMICILIARY/ DOMICILIARYto TZS | NIL | NIL |
| SECTION ( | DEPOSIT ACCOUNTS | | |
| 1 | Call Accounts | | Call Accounts |
| | Minimum opening balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Monthly Average balance requirement | Negotiable | Negotiable |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| 2 | Term Deposits | | Term Deposits |
| | Minimum deposit - local currency | TZS 500,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum deposit - USD | USD 1,000 | USD 10,000 or equivalent |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| SECTION I | ELECTRONIC BANKING | | |
| 1 | E-Banking | | E-Banking |
| | Internet banking monthly subscription | TZS 2,000 Per Month. | TZS 10,000 per Month |
| | Internet banking ( Re issue pin) | FREE | FREE |
